Nipashe
Jumanne Julai 21, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580289
The Guardian digital
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



USICHUKULIE POA NYUMBA NI CHOO
Kaa kwa kuachiana nafasi hatua 2 au 3
2 mtr
USICHUKULIE POA UNATEGEMEWA

## Ahukumiwa kufungwa maisha kwa kumbaka mtoto miaka 5 mfululizo

UKURASA 4

# Vigogo wang'ara kura za maoni ubunge CCM

**WASANII**, wanahabari waambulia kiduchu, vituko vyatawala kila kona, Magufuli asisitiza uwazi, Kilolo wachelewa kuanza uchaguzi kisa...

*Endelea uk. 2,3,7 na 8*

**WALIOONGOZA**


Alexander Mnyeti


Dk. Faustine Ndugulile



Dk. Tulia Ackson


Livingstone Lusinde


Prof. Kitila Mkumbo


Spika Job Ndugai


Tarimba Abbas


Mrisho Gambo

**WALIOSHINDWA**


Agrey Mwanri


Charles Kitwanga


Dk. Charles Kimei


Joshua Nassari


Maulid Mtulia


Paul Makonda

## JPM asema Tanzania iko shwari watalii wamiminika

UKURASA 2



Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store

MICHEZO SABA ZACHUNGULIA SHIMONI LIGI BARA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



Rais John Magufuli akimwapisha Marwa Mwita Rubirya kuwa Mkuu wa Mkoa wa Njombe katika Ikulu ya Chamwino, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Vigogo wapeta kura za maoni CCM

**Na Waandishi Wetu**

MCHAKATO wa kura za maoni kuwasaka wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) watakaopeperusha bendera ya chama hicho kusaka ubunge na uwakilishi ulianza jana, baadhi ya vigogo wakiendelea kung'ara.

Miongoni mwa vigogo waliong'ara ni Spika wa Bunge, Job Ndugai na Naibu wake, Dk. Tulia Ackson.

Kenye Jimbo la Kongwa, Spika Ndugai ameongoza akipata kura 850 akifuatwa na Dk. Samora Mshanga aliyepata kura 20, Isaya Mngulumi (19), Dk. Philimon Saigod (6), Neemia Chibelenje (2), Apiov Iwiwa (1) na Morice Zaid (0).

Wakati Ndugai akiongoza, mjini Mbeya naibu wake, Dk. Tulia naye aliwazidi kete washindani wake 31 akiongoza kwa kura 843 kati ya 924 zilizopigwa, akifuatwa na Dk. Mahande Mabula aliyepata kura 16 na Charles Mwakipesile aliyepigiwa kura 11.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Seleman Jafo, alipata kura 588 kati ya 601 zilizopigwa, akifuatwa na Dk. Zemba Mumbi, Salum Cahurembo, Ally Goha na Zainab Adam walioambulia kura mbili kila mmoja.

Vilevile, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kapteni mstaafu George Mkuchika, ameongoza kwa kura 319 kwenye Jimbo la Newala mkoani Mtwara akifuatwa na Rashid Mtima (121) na Karimu Lichela (42).

Luhaga Mpina, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naye ameibuka mshindi kwenye mchakato huo wa maoni kwa kupata kura 316 kati ya 486 zilizopigwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Jimbo la Kisesa.

Akitangaza matokeo hayo jana Makao Makuu ya Jimbo la Kisesa Mjini Mwandoya, Msimamizi wa Uchaguzi huo, Mayunga George, ambaye ni Katibu Mwenezi wa CCM Mkoa wa Simiyu, alisema jumla ya kura zilizopigwa ni 486 na Mpina alipata kura 316.

Wagombea wengine waliomfuatia ni Mussa Mbuga kura 152, Itandula Gambamala (9), Mlasi Kichamo (4), Lazaro Magumba (2), Madili Mlasi (2), Silinde Nchachile (1) huku wagombea wengine walioshiriki wakipata kura sifuri.

Wakati Mpina aking'ara Kisesa, Naibu wake, Abdallah Ulega, ameongoza katika Jimbo la Mkuranga akipata kura 1,138, akifuatwa na Ramadhan Mlao (50) na Ally Mawe (7).

Katika Jimbo la Ilala jijini Dar es Salaam, kati ya kura 278 zilizopigwa, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, alipata kura 148, akifuatwa na Sophia Mjema aliyepata kura 103.

Wakati Zungu aking'ara Dar es Salaam, Naibu wake, Mussa Simba, ameongoza kwa kura 158 kuwania kuteuliwa Jimbo la Sindiga Mjini, akifuatwa na Charles Kisuke (124) na Hassan Mazala (92).

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, pia ameongoza kwa kura 667 katika Jimbo la Kibakwe, akifuatwa na Kwame Mwaga (151).

Katika Jimbo la Nzega Mjini lililokuwa na watia nia 12, Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, anayetetea kiti chake cha ubunge, ameongeza kwa kupata kura 376 akifuatwa na Mashili Petro aliyepata kura sita.

Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Awesso, pia ameibuka kinara katika kura hizo Jimbo la Pangani mkoani Tanga, akipigiwa kura 282, huku Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, aking'ara Jimbo la Ilemela kwa kura 502 akifuatwa na Israel Mtambalike (112) na Nkilila Lucas (13).

Katika Jimbo la Kinondoni jijini Dar es Salaam, mwanamichezo Abbas Tarimba, ameongoza akipigiwa kura 171, akifuatwa na aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo katika Bunge la 10, Iddi Azan (77), George Manyama (38), huku aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo katika Bunge la 11, Mauld Mtulia akiambulia kura 11 na Mtangazaji Zamaradi Mketema akipata kura mbili.

Kwenye Jimbo la Chalinze, Ridhiwan Kikwete, mtoto wa Rais wa awamu ya nne, Dk. Jakaya Kikwete, ameongoza kwa kura 369 akifuatwa na Ramadhan Maneno (273) na Said Zikatimu (223).

Wilayani Kahama mkoani Shinyanga, Naibu Waziri wa Ujenzi, Elias Kwandikwa, ameongoza kwa kura 730 katika kulisaka Jimbo la Ushetu, akifuatwa na Mlyase Kikuli (57) na Emmanuel Peter (46).

Wilayani Ubungo jijini, aliyekuwa Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Dk. Kitila Mkumbo, ameongoza kwa kupigiwa kura 172 kwenye Jimbo la Ubungo akifuatwa na Mwatuma Mgonja aliyepata kura 73.

Mwanasheria Mkuu wa zamani wa serikali, Andrew Chenge' ameongoza kwa kura 442 Jimbo la Bariadi, akimzidi kete Kundo Mathew aliyepata kura 339.

Aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mohamed Mchengerwa ameongoza kwa kura 273 kuwania kuteuliwa Jimbo la Rufiji mkoani Pwani, akifuatwa na Dk. Seif Rashid (120) na Athuman Likeikei (62), huku Dk. John Palangyo akiongoza Arumeru Mashariki kwa kura 536.

Wakati hali ikiwa hivyo Rufiji, aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Peter Serukamba, amenga'ra Kigoma Kaskazini, akipata kura 261 dhidi ya kura 81 za Assa Makanike na 51 za Suleiman Hanzuruni.

## Watalii wamiminika Tanzania

**Na Mary Geofrey**

RAIS John Magufuli amesema idadi ya ndege zilizobeba watalii inaendelea kuongezeka nchini baada ya kumalizika kwa ugonjwa wa corona ulioingia nchini Machi 16 mwaka huu.

Amesema Tanzania sasa iko salama na watendaji waendelee kutangaza hilo kwa sababu ugonjwa wa corona umemalizwa kwa njia ya kumwomba Mungu.

Rais Magufuli aliyaeleza hayo jana Ikulu Chamwino jijini Dodoma, muda mfupi baada ya kuwaapisha viongozi walioteuliwa kushika nafasi mbalimbali za uongozi nchini.

"Nimeanza kuona ndege za watalii zinakuja nyingi na idadi ya watalii inaongezeka, watu wameshaanza kuangalia na kuuona ukweli, kwamba hapa Tanzania tupo salama," alisema Rais Magufuli.

"Tupo salama na endeleeni kulitangaza hili, maadui zetu watazungumza mengi, lakini Tanzania tupo salama. Hata hapa tungekuwa tumevaa barakoa, lakini hakuna aliyevaa hapa, ni kwa sababu tupo salama. Kwani sisi hatuogopi kufa?" alihoji.

Rais Magufuli aliendelea kusema kuwa corona ipo mbali na kwamba ilimalizwa kwa maombi ambayo Watanzania waliamua kumwomba Mungu.

"Tuliamua kumwomba Mungu, tukamtanguliza Mungu na akatusikia. Tanzania tupo salama na ninyi endeleeni kuitangaza Tanzania iko salama, watalii waje na kila mtalii atakayekuja ataangalia wanyama wake na atarudi akiwa salama," alisisitiza Rais Magufuli.

Kiongozi huyo wa nchi pia alimpongeza Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii (TTB), Jaji Thomas Mihayo, kwa kazi kubwa wanayofanya kuhakikisha idadi ya ndege za watalii zinaongezeka nchini.

"Ninakushukuru Mheshimiwa Jaji Mihayo na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kazi kubwa mnayofanya, nimeanza kuona watalii wengi wanakuja na ndege za watalii zikiendelea kuongezeka nchini," alisema Rais Magufuli.

HABARI KITAIFA

## Vigogo walioanguka kura za maoni CCM

**Na Waandishi Wetu**

MCHAKATO wa kura za maoni ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ulioanza jana, unatarajiwa kuhitimishwa leo, huku baadhi ya vigogo wakianguka.

Miongoni mwa walioanguka, yumo aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Dk. Charles Kimei, na aliyekuwa Mbunge wa Misungwi, Charles Kitwanga.

Mkoani Kilimanjaro, jana kulishuhudiwa katika Jimbo la Vunjo Dk. Kimei akishika nafasi ya pili kwa kura 178 nyuma ya kinara Zadock Koola aliyepata kura 187.

Wilayani Kondoa mkoani Dodoma, aliyekuwa Mbunge wa Kondoa Mjini, Edwin Sannda, ameanguka katika kura hizo baada ya kuambulia kura 24 dhidi ya Ally Makoa aliyeongoza, akifuatwa na Omary Kimbisa (71).

Mkoani Geita, aliyekuwa Mbunge wa Mbogwe katika Bunge lililopita, Augustino Masele, ameanguka katika kura hizo baada ya kupigiwa kura 212 dhidi ya 265 alizopata Nicodemas Maganga. Patrick Msafiri ameshika nafasi ya tatu kwa kura 16.

Mkoani Katavi, Jimbo la Simbo limevutia makada 16 wa CCM akiwamo aliyekuwa mbunge wake katika Bunge la 11, Richard Mbogo, ambaye ameanguka baada ya kupata kura 121 dhidi ya 355 za aliyekuwa mbunge wa viti maalum, Anna Lupembe.

Mjini Moshi, Ibrahim Shayo ameongoza kwa kura 140 dhidi ya Pricus Tarimo (137) na Beno Malisa, huku Noel Severe akiongoza Arumeru Magharibi kwa kura 113 akifuatwa na Joseph Lukumai (66) na David Sigara (59) huku aliyekuwa mbunge wake, Goodluck Olimedey akiambulia kura 14.

Wakati hali ikiwa hivyo mjini Moshi, mkoani Arusha, aliyekuwa Mbunge wa Longido, Steven Kiruswa, ameongoza kwa kura 529 dhidi ya 68 na 45 za Mwalimu Lomayan Logolle na Sabore Kennedy, mtawalia.

Aliyekuwa Mbunge wa Morogoro Mjini katika Bunge lililopita, Abdulaziz Abood, ameongoza katika kura hizo akipigiwa kura 524 na kuwazidi kete Merkiory Manset (17), Ally Simba (15) na Iddah Omary (10).

Mkoani Dodoma, Livingstone Lusinde, ameongoza katika kura hizo kwa kupigiwa kura 571 dhidi ya 122 na 37 za Dk. Michael Msendekwa na Mwanga Chibago, mtawalia.

Mkoani Kigoma, aliyekuwa Katibu wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam, Kirumbe Ng'enda, ameongoza kwa kura 218 Kigoma Mjini akifuatwa na Juma Mwaka (44) na James Rudonya (37).

Jimbo la Magu lilivutia makada 45 huku aliyekuwa mbunge wake, Boniventura Kiswaga, akiongoza kwa kura 486 akifuatwa na Noel Mabula (76).

Katika Jimbo la Rombo mkoani Kilimanjaro, aliyekuwa Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Profesa Adolf Mkenda, ameongoza kwa kura 285 dhidi ya 87 za Anthony Mseke na Samora Kanje (31).

# JPM afunguka mafuriko watia nia ubunge CCM

**Na Mary Geofrey**

RAIS John Magufuli amesema idadi kubwa ya wanachama waliojitokeza kuwania nafasi za ubunge na uwakilishi kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), ilikuwa haijawahi kutokea ndani ya chama hicho.

Amesema idadi ya wanachama 10,367 walichukua fomu za kuomba kuteuliwa kuwania nafasi ya ubunge na uwakilishi na kati yao, 10,321 walikamilisha taratibu na kurudisha fomu.

Muda mfupi baada ya kuapishwa kwa viongozi walioteuliwa mwishoni mwa wiki, Rais Magufuli alisema Ikulu Chamwino, Dodoma jana kuwa, watia 46 hawakurudisha fomu hizo.

"Kwa hiyo mnaweza kuona ni watu wengi sana waliojitokeza, haijawahi kutokea, haijawahi kutokea, kwamba katika chama kimoja, wagombea kwenye kiti cha ubunge, bado udiwani, kwenye ubunge tu 10,367.

"Nami ninawapongeza sana wote waliojitokeza kwenda kuomba nafasi mbalimbali kwenye chama chetu, Chama Cha Mapinduzi," alisema Rais Magufuli.

Alisema ana matumaini kuwa kura za maoni zilizoanza jana na kutarajiwa kumalizika leo, zitasimamiwa kwa uwazi bila mizengwe, ili kila mwenye haki apate haki yake.

"Na mimi ningetamani sana viongozi wa chama changu ambao watasimamia uchaguzi huu kwa leo (jana) na kesho (leo), kura zikishapigwa, ifanyike kama ilivyofanyika kwenye Halmashauri Kuu ya CCM, zihesabiwe kwa uwazi hadharani, anayepata zero (sifuri), aipate hapohapo, anayepata zote iwe pale pale," aliagiza.

Rais Magufuli alisisitiza kuwa, uwazi huo utaendelea kujenga umoja wa wanachama wa CCM.

"Kwa hiyo viongozi wenzangu wa CCM, nitafurahi sana kuona kura hizi zinahesababiwa hadharani mbele ya wajumbe, ili kila mmoja ajue alichopata na hii ndiyo demokrasia na kukua kwa demokrasia," alisema.

Vilevile, Rais Magufuli aliwataka wateule aliowaapisha kwenda kufanya kazi kadri ya uwezo wao na kushirikiana na viongozi wengine watakaowakuta katika maeneo waliyopangwa.

"Kama wewe ni DAS (Katibu Tawala wa Wilaya), nenda kafanye kazi ya uDAS kwa kushirikiana na makatibu tarafa, watendaji wa kata na wengine wenyeviti wa vijiji na kadhalika katika kutatua matatizo ya wananchi kule.

"Kama wewe ni DED kashukughulikie matatizo kwenye halmashauri, kasimamie miradi kikamilifu pasiwapo na miradi hewa na kadhalika. Kama wewe ni DC hivyo hivyo, kama wewe ni RAS hivyo hivyo, kama wewe ni Naibu Katibu Mkuu kafanye hivyo hivyo, kama wewe ni Katibu Mkuu hivyo hivyo, nendeni mkashirikiane na viongozi wengine katika kuitengeneza nchi yetu," aliagiza.

Rais Magufuli pia alisema ana imani kuwa wateule hao wapya hawataacha nafasi zao kwenda kusaka nafasi nyingine zikiwamo za kupigiwa kura, na kwamba hatafanya tena uteuzi wa viongozi wengine hadi hapo uchaguzi utakapokamilika.

Baadhi ya wateule walioapishwa na Rais Magufuli jana ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Mwinyi Talib Haji, na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Marwa Mwita Rubirya.

Viongozi wengine ni Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe, Dk. Seif Shekilag, Mkuu wa Wilaya ya Ilala mkoani Dar es Salaam, Mussa Ramadhani Chogelo na Mkuu wa Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu, Aswege Enock Kaminyonge.

Wengine ni Mkuu wa Wilaya ya Kalambo mkoani Rukwa, Calorious Misungwi, Mkuu wa Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro, Dk. Athuman Kihamia, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo mkoani Iringa, Lainie Ephaim Kamendu, Katibu Tawala wa Wilaya ya Arusha, Hanan Mohamed Bafagil.



Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mussa Azzan Zungu (katikati mwenye miwani), akipongezwa na wanachama wa CCM, baada ya kuongoza katika kura za maoni za kuomba kuteuliwa kugombea ubunge wa Jimbo la Ilala, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Makonda aanguka, Gambo apeta

## ■Kura moja shida kwa Mwanri

**Na Waandishi Wetu**

ALIYEKUWA Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, ameanguka kwa kura moja katika mchakato wa kuteuliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwania ubunge wa Jimbo la Siha mkoani Kilimanjaro.

Vilevile, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ameanguka katika kura hizo za maoni ndani ya CCM baada ya kuzidiwa kete na aliyekuwa Naibu Waziri wa Afya, Dk. Faustine Ndugulile kusaka Jimbo la Kigamboni.

Katika jimbo hilo, kura 399 zilipigwa kuwachuja makada 178 waliokuwa wamejitokeza, Dk. Ndugulile akipata kura 190 dhidi ya 122 za Makonda.

Baadhi ya wagombea, akiwamo mchekeshaji Mpoki, hawakupata hata kura moja kutoka kwa wajumbe wa mkutano mkuu wa jimbo.

Wilayani Siha, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, ameongoza akipigiwa kura 148 akifuatwa na Mwanri aliyepata kura 147 na Tumsifu Kweka (53).

Mkoani Mwanza, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, amepata kura 406 na kumbwaga aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Charles Kitwanga, aliyepata kura 260 katika kinyang'anyiro cha Jimbo la Misungwi.

Mjini Arusha, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, ameongoza kwa kupata kura 333 kati ya 478, akifuatwa na Philemon Mollel (68) na Wakili Albert Msando (19).

# Jela maisha kwa kubaka mwanafunzi miaka mitano

**Na Joctan Ngelly, KIGOMA**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kigoma imemhukumu mkazi wa Katubuka Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Jeremia Kilahunja (49), kifungo cha maisha jela kwa kubaka mwanafunzi wa shule ya msingi kwa miaka mitano tangu akiwa na umri wa miaka sita.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Katoki Mwakitalu, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha makosa matano yaliyokuwa yakimkabili.

Hakimu Mwakitalu alisema mahakama inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa watu wengine wenye tabia kama hiyo.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Raymond Kimbe, ulipeleka mahakamani mashahidi wanne na kielelezo kimoja cha PF3, ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alimbaka mwanafunzi huyo mara tano.

Kadhalika, alisema siku ya tukio mwanafunzi huyo alikuwa akirudi kutoka shuleni na kumkuta mshtakiwa akipalilia shamba karibu na nyumbani kwao na alipomwona alimuita na kumwomba akamnunulie chakula ndipo mwanafunzi huyo alipoenda nyumbani na kubadilisha nguo na kumfuata mshtakiwa ili akachukue pesa ya kununua chakula hicho.

Alisema baada ya mwanafunzi huyo kuondoka, mshtakiwa alimuita na kumwambia kuna kitu amesahau na aliporudi alimkamata na kumpeleka kwenye vichaka na kumwamuru avue nguo na kuanza kumbaka huku akimtishia kumcharanga panga kama atamwambia mtu kuhusu tukio hilo.

Mwakitalu alisema mshtakiwa huyo mara ya kwanza alimbaka mwanafunzi huyo akiwa na umri wa miaka sita mwaka 2015, mara ya pili mwaka 2016, mara ya tatu mwaka 2017, mara ya nne mwaka 2018 na mara ya tano mwaka 2019.

Alisema mara ya tano mshtakiwa alimkuta mwanafunzi huyo akiwa na mdogo wake wanachunga mbuzi maeneo ya Airport, alimuita na kumpeleka vichakani na kuanza kumbaka. Mdogo wake aliyekuwa naye alikuwa akiwachungulia na mbakaji alipomaliza kufanya tukio hilo la kinyama, watoto hao walirudi nyumbani.

Hakimu alisema, walipofika nyumbani mdogo wa mwanafunzi huyo alimwambia mama yake tukio lililotokea wakati wakiwa wanachunga.

Alisema mama yake alimchukua mtoto wake hadi kituo cha polisi na kupewa PF3 kwa uchunguzi na daktari alithibitisha mwanafunzi huyo hakuwa na bikira na ilionekana kufanyiwa kitendo kwa muda mrefu.

Hakimu Mwakitalu alisema upande wa mashtaka umethibitisha makosa yote matano na kumtia hatiani kwa makosa yote.

Katika tukio la kushangaza, mshtakiwa alipotakiwa kujitetea, aliangua kilio na kuomba mahakama imfikirie kwa kuwa mtoto mdogo anapobakwa lazima damu itatoka na atibiwe.

Hakimu Mwakitalu alitoa adhabu kwa kosa la kwanza kwenda jela maisha, kosa la pili a jela maisha, kosa la tatu jela maisha, kosa la nne jela maisha na kosa la tano jela miaka 30, lakini makosa yote yanakwenda pamoja hivyo atatumikia kifungo cha maisha jela.

Awali, akisoma hati ya mashtaka Wakili wa Serikali Raymond Kimbe, alidai tarehe isiyofahamika mwaka 2015 eneo la Airport Manispaa ya Kigoma/Ujiji, mshtakiwa alimbaka mwanafunzi akiwa na umri wa miaka sita. Tarehe isiyofahamika mwaka 2016 alimbaka tena mwanafunzi huyo akiwa na umri wa miaka saba. Tarehe isiyofahamika mwaka 2017 maeneo ya Katubuka mshtakiwa alimbaka mwanafunzi huyo akiwa na miaka minane.

Pia, tarehe isiyofahamika mwaka 2018 maeneo ya Katubuka mshtakiwa alimbaka mwanafunzi huyo akiwa na miaka sita na mwaka 2019 maeneo ya Jusi, mshtakiwa alimbaka mwanafunzi huyo akiwa na miaka 10 kinyume cha sheria.



Mkazi wa Katubuka Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Jeremia Kilahunja (49), akiwa chini ya ulinzi wa polisi katika Mahakama ya Wilaya ya Kigoma jana, baada ya kuhukumiwa kifungo cha maisha jela kwa makosa matano ya kubaka mwanafunzi. **PICHA: JOCTAN NGELLY**

## Wajasiriamali kilimo kunufaika na mikopo

**Na Mwandishi Wetu, MTWARA**

WAJASIRIAMALI katika sekta ya kilimo nchini, hivi sasa wanayo fursa ya kugeuka wazalishaji wakubwa kutokana na mageuzi waliyofanyiwa kuwafungulia milango kufikia upeo huo, imeelezwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya PASS, ambayo inawajibika na mageuzi hayo, Nicomed Bohay, alitamka hayo mjumuiko wa kimafunzo mkoani hapa unaolenga kuwajengea wadau husika kufikia upeo huo, baada ya Benki Kuu (BoT) kuipatia baraka fursa hiyo ya kiutendaji.

Aliitaja fursa hiyo mpya ni ya huduma za kifedha, itakayopatikana kupitia kampuni mpya inayoitwa PASS Leasing company LTD, inayomilikiwa na PASS, itatoa huduma ya kuwakopesha wajasiriamali hao wa kilimo.

"Tutawajengea mazingira rahisi zaidi kwa wakulima kumiliki nyenzo za kisasa za kilimo," alisema Bohay katika tukio hilo lililowajumuisha mamia ya wadau mjini hapa.

Lengo la kampuni ni kuisadia sekta ya kilimo kwa kufanikisha mikopo kuhakikisha wakulima wanazalisha kwa kiwango kikubwa baada ya kubaini wengi wao wanazalisha mazao chini ya kiwango.

"Kupitia mfumo huu, tunakwenda kuwarahisishia wakulima kupata zana za kisasa za kilimo ili waachane na kilimo cha kizamani cha kutumia zana duni za kilimo," alisema Bohay.

Killo Lussewa, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo mpya, alisema itatoa huduma ya dhamana kwa wajasiriamali ambao wamekuwa wakikosa mikopo kwa kukosa dhamana na hivyo kutokushiriki kikamilifu katika mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo.

"Hii ni fursa muhimu kwetu kuonyesha kuwa kuna soko kubwa kwenye kilimo na kuhamasisha uwekezaji mkubwa zaidi kwenye sekta hii ili taasisi nyingine za kifedha ziione na kusaidia wakulima," Lussewa alisema.

Asasi hiyo imekuwa ikishirikiana na taasisi nyingine za kifedha zikiwamo benki za CRDB na TIB kusaidia wakulima na wajasiriamali katika sekta ndogo ya kilimo biashara.

Kwa mujibu wa BoT, kati ya mikopo 8,285,831 iliyotolewa na benki kwa sekta ya kilimo kati ya mwaka 2013 na 2019, mikopo 956,298 ilikuwa chini ya udhamini wa PASS.

# Shule yaomba kufungiwa umeme

**Na Tiganya Vincent**

SHULE ya Sekondari Mwanhala wilayani Nzega imeliomba Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuwaunganisha na mtandao wa umeme kuwawezesha wanafunzi kupata mazingira mazuri ya kujisomea nyakati za usiku.

Ombi hilo lilitolewa jana na Makamu Mkuu wa Shule hiyo, Malugu Kusolwa, wakati akitoa taarifa ya ujenzi wa bwalo la chakula na ukamilishaji wa maabara mbili kwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, aliyekuwa katika ukaguzi wa miradi ya maendeleo.

Alisema ukosefu wa umeme katika shule hiyo kongwe umeathiri ufaulu wa wanafunzi kwa kuwa wamekuwa wakitumia taa ambazo zina mwanga hafifu na wameshindwa kutumia mwingi kujisomea.

Katika hatua nyingine, Makamu Mkuu huyo wa Shule aliishukuru serikali kwa kuwapa Sh. milioni 150 kwa ajili ya ujenzi wa bwalo la chakula na ukamilishaji vyumba viwili vya maabara ya baiolojia na kemia za shule hiyo.

Alisema ujenzi wa bwalo la chakula hadi hivi sasa umegharimu Sh. milioni 103.2 na ukamilishaji wa vyumba viwili vya maabara umegharimu Sh. milioni 50.

Kusolwa alisema kujengwa kwa bwalo hilo kutasaidia wanafunzi kupata chakula katika mazingira salama na yenye utulivu pamoja na kuwa na eneo la kufanyia mikutano na sherehe za shule.

Alisema bwalo litawawezesha wanafunzi kuwa na eneo la kujisomea nyakati za usiku na eneo la kufanyia mitihani ya kitaifa.

Akijibu maombi hayo, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, alimwagiza Meneja wa TANESCO Wilaya ya Nzega kuhakikisha shule hiyo inapata umeme wa REA, ili kuwawekea mazingira mazuri wanafunzi ya kujifunza nyakazi za usiku na kuimarisha usalama wa shule.

HABARI KITAIFA

# Uagizaji mafuta wavutia nchi jirani

Na Joseph Mwendapole

MFUMO wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja Bulk Procurement, umeelezwa kuonyesha mafanikio na kuzivutia nchi jirani kuja kujifunza namna ya kuuendesha.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi wa Wakala wa Uagizaji Mafuta (PBPA), Erasto Mulokozi.

Alisema mfumo huo umesaidia kuwa na uhakika wa mafuta ya kutosha kwa kipindi chote na kushusha gharama za uagizaji, hivyo kumpunguzia gharama mlaji wa mwisho.

Alisema kutokana na mafanikio hayo, Zambia, Uganda, Malawi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) zimekuwa zikituma maofisa wake kuja kujifunza namna wanavyoweza kuutumia ili kupunguza gharama za uagizaji.

Alisema hata taasisi zingine za serikali zimeanza kuiga mfumo huo ikiwamo mbolea ambapo taasisi hiyo imewapa wataalamu wake wawape mafunzo kuufahamu mfumo huo.

Aidha, alisema mfumo huo umesaidia kupunguza msongamano wa meli ambazo awali zilikuwa zikikaa hadi siku 60 kusubiri kushusha mafuta, hivyo kuongeza gharama za nishati hiyo kwa mtumiaji wa mwisho.

Alisema uagizaji wa pamoja umeondoa kero hiyo kwani hivi sasa meli yenye shehena ya mafuta hukaa bandarini ikipakua mafuta kwa wastani wa siku tatu pekee.

"Kwa kawaida meli inapozidi kukaa kusubiri kushusha mafuta inatoza gharama za ucheleweshwaji hivyo wenye kampuni za mafuta walikuwa wakifidia gharama hizo kwa kumwongezea bei mlaji wa mwisho," alisema Mulokozi.

Alisema mfumo wa uagizaji wa pamoja umekuwa ukisaidia kupata mafuta kwa bei nafuu kuliko ilivyokuwa zamani na ndiyo sababu bei ya nishati hiyo imekuwa chini kwa muda mrefu.

Mulokozi alisema mfumo huo umewezesha kupatikana kwa takwimu sahihi za mafuta yanayoingizwa nchini, hivyo kuirahishia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kujua kiasi cha kodi inachotakiwa kuchukua.

Alisema kuna taasisi zingine ambazo zikitoza tozo za maji, umeme na barabara hivyo wamekuwa wakitumia takwimu hizo kujua kiasi cha fedha wanazotakiwa kupata.

"Mbali na kuisaidia nchi kupata takwimu sahihi za mafuta yanayoingia pia tuna uhakika wa kuletewa mafuta bora kwa sababu kabla ya meli yetu kushusha mzigo tunawaita TBS kuthibitisha na wakitupa majibu ndipo tunawaambia washushe mzigo," alisema.




Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), Mhandisi Japhet Maselle (kushoto), Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wakala huo, Prof. Idrissa Mshoro (katikati) na Mkurugenzi wa Kampuni ya Songoro, Major Songoro wakipita kukagua maendeleo ya ujenzi wa kivuko cha MV Ukara, katika yadi ya Songoro Ilemela, jijini Mwanza jana. Kivuko hicho, kinachotarajiwa kukamilika Agosti mwaka huu, na kitatoa huduma kati ya Bugorola na Ukara. **PICHA: WUUM**

# Shule zapewa somo kuweka mfumo wa kuzuia majanga

Na Joseph Mwendapole

SHULE nchini zimeshauriwa kuweka mifumo thabiti ya kuzuia majanga ya moto na kuweka vifaa vya kisasa vya kuzimia moto, ili kuwahakikishia usalama wanafunzi wanaosoma kwenye shule hizo.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Shule ya St. Anne Marie Academy ya Mbezi kwa Msuguri, jijini Dar es Salaam, Gladius Ndyetabura, wakati wa mahafali ya 12 ya kidato cha sita yaliyofanyika kwenye viwanja vya shule hiyo.

Alisema shule hiyo inajivunia kuweka mifumo mizuri ya kuwahakikishia usalama wanafunzi wake kwani wamefanikiwa kuweka vifaa vya kisasa vya kuzimia moto na ina askari wenye mafunzo na uzoefu wa kuzima moto endapo utatokea kwenye shule hiyo.

"Kumekuwa na majanga ya kuungua kwa mabweni kwenye shule, hivyo shule zinawajibika kufanya kama St Anne Marie kwa kuweka vifaa vya kisasa na kuwapa mafunzo askari wake kuwa tayari wakati wowote janga hilo likitokea," alisema.

Alisema wanafunzi wote waliohitimu kidato cha sita mwaka 2019, walijiunga na vyuo vikuu mbalimbali ndani na nje ya nchi na 40 waliopata ufaulu mzuri zaidi walipata ufadhili wa kwenda kusoma China, India na Canada.

Mkuu huyo alisema wanafunzi wanaohitimu kidato cha sita wako 200 na wameandaliwa vya kutosha na walimu makini kwa kufanya mazoezi mengi na imani yake ni kwamba wote watafaulu kwa daraja la kwanza.

Alisema katika mitihani ya Mock wanafunzi wote hao walipata daraja la kwanza na la pili pekee na hakukuwa na daraja la tatu, la nne wala 0 na imejipanga kwa kushirikiana na wazazi kuhakikisha wanapata vyuo vikuu vizuri ndani na nje ya nchi.

"Shule kwa kushirikiana na wazazi itafanya jitihada kuhakikisha wanasomea kozi nzuri zitakazowasaidia kupata fursa ya ushindani kwenye soko la ajira ndani na nje ya nchi na kupata mikopo," alisema.

Pia alimshukuru mwanzilishi wa shule hizo, Dk. Jasson Rweikiza, kwa ujasiri wake wa kuwekeza kwenye elimu na kuwekeza kwenye miundombinu bora kuhakikisha wanafunzi wanasomea kwenye mazingira mazuri na kwamba hiyo ndiyo siri ya mafanikio ya shule hiyo mwaka hadi mwaka.

## PM asisitiza ulinzi shirikishi

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema suala la ulinzi wa nchi ni la Watanzania wote na siyo la kuachia vyombo vya ulinzi pekee kama Jeshi la Wananchi, Uhamiaji, Polisi au Magereza.

Ametoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na wakazi wa Matogoro wilayani Tandahimba, mkoani Mtwara.

"Suala la ulinzi ni letu sote na siyo la serikali peke yake kupitia wanajeshi au polisi. Kila Mtanzania anawajibika kuilinda nchi hii, kuanzia nyumbani kwako hadi kwa jirani yako. Niwakumbushe kwamba tunapaswa tuendelee kujenga utamaduni wa kutoa taarifa, kila unapoona kuna jambo ambalo una shaka nalo," alisema.

Alisema mikoa ya pembezoni ya Kigoma, Kagera, Mtwara, Ruvuma, Katavi, Songwe, Mbeya, Lindi, Mara, Tanga, Kilimanjaro na Arusha, wananchi wake ni lazima wawe wepesi wa kutoa taarifa. "Ni lazima Watanzania tuwe makini, hata kama tuna utaratibu wa kutembeleana, ni lazima tuwe macho."

Kadhalika, alisema serikali imeweka mwongozo kwa wageni wanaoingia nchini ambao ni lazima apite kwenye mpaka ulio rasmi na kutoa taarifa zake. "Mgeni huyo atapaswa aeleze amekuja nchini kufanya nini, amekuja na nani na atakaa kwa siku ngapi."

"Tunapomwona mgeni huko kijijini, ni lazima tujiridhishe kuwa mgeni huyo amepitia kwenye sehemu zote husika. Kama mtu utaona shaka, toa taarifa kwa mtendaji naye atapeleka taarifa hizo ngazi za juu hadi kwa Mkuu wa Wilaya."

Alisema kila mwananchi atakapojiridhisha kuwa nchini kuna amani, kutakuwa na hali ya utulivu ambayo ni muhimu kwa usalama wa ndani na nje.

Waziri Mkuu alisema wilaya za Masasi, Nanyumbu na Mtwara Vijijini ni maeneo yanayovutia watu kuingia nchini kwa sababu ya zao la korosho na biashara zilizopo. "Hapa Tandahimba kuna mzunguko mkubwa wa fedha. Tandahimba ina idadi kubwa ya wafanyabiashara, hivyo ni rahisi kwa mtu kuja kufanya ujambazi au kuiba mazao yenu. Tunataka muwe macho, lengo letu ni kuhakikisha eneo hili lisiwe moja ya maeneo hatarishi," amesisitiza.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Matukio moto shuleni yanahitaji ufumbuzi*

NI matukio endelevu yenye simanzi kuhusiana na mikasa ya athari na vifo kutokana na ajali za zimamoto kutokea katika shule mbalimbali nchini kila wakati.

Hivi sasa kinachotawala ni simulizi ya moto wenye athari kubwa katika Shule ya Sekondari Kinondoni Muslim ya jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki iliyopita.

Ikiangaliwa kwa kina, ni janga linalosikitisha zaidi kwa mtazamo kuna ajali kama hiyo yenye athari za mali, afya na vifo vya wanafunzi, wiki mbili kamili zimepita katika shule nyingine ya sekondari iliyoko Ilala, Dar es Salaam, kabla ya hilo lililotokea Kinondoni.

Kimsingi, katika sura pana ni aina ya matukio mabaya yasiyokoma katika shule mbalimbali na mahsusi kwenye mabweni, ambayo ndiyo makazi ya wanafunzi wanaoishi shuleni.

Hiyo inachukua sura inayotawala huku kukifahamika kwamba shule mbali na kubeba jukumu la kufundisha, kwa wakati wote inabeba majukumu ya wazazi au walezi wa watoto na mengine kwa maelekezo ya serikali.

Katika mwendelezo wa matukio hayo ya simanzi, Oktoba mwaka jana itakumbukwa mkasa wa kuungua mabweni ya shule moja ya sekondari mkoani Mbeya, hata ikatawala hisia za kitaifa. Pia mwaka 2016 mkoani humo mabweni ya shule nyingine yaliungua.

Matukio kama hayo kitaifa ni mengi, kwani kukirejewa mwaka 2016 kwenye shule ya sekondari iliyopo wilayani Monduli, pia mkoani Morogoro mwaka 2012, mabweni ya wasichana yaliungua.

Hapana shaka bado kubwa katika lote ni rekodi inayogusa Shule ya Sekondari Shauritanga, mkoani Kilimanjaro iliyotikisa nchi nzima mwaka 1994, wanafunzi wengi waliungua bwenini na kupoteza maisha, hata wakazikwa katika makaburi ya pamoja shuleni hapo.

Kwa kurejea picha hiyo ya matukio ya moto yanayojiri katika mazingira endelevu ya shule mbalimbali nchini na kwa namna ya pekee bweni, kuna haja ya umma kujiuliza kulikoni matukio haya ya moto yanayojirejea kila mara?

Shule ni hatua mojawapo ya ulezi katika umma kwa kila nchi. Pia, ikiangalia kwa kina, elimu ya msingi nchini ni hatua ya lazima kisheria ambayo mtoto anapaswa kupitia.

Aidha, katika maisha ya kila siku, hata kwa wanafunzi anayeishi nyumbani, bado wastani kati ya theluthi na nusu ya siku yake, hutawaliwa katika harakati za masomoni, kwa hatua za kwenda na kurudi na mahudhurio masomoni.

Hiyo maana yake ni nini? Maisha ya mwanafunzi yanagawanyika kati ya shule na nyumbani. Anapoondoka nyumbani, dhamana inaangukia shuleni ambako waangukia dhamana ya pii, walimu na wasimamizi wengine wakibeba jukumu la uzazi.

Huko shuleni, tafsiri pana ya ulezi inajumuisha usalama, kama ilivyo majumbani wanakopatikana wazazi, jitihada zinafanyika kuwaweka salama dhidi ya hatari kama vile matukio ya moto. Hicho ndicho kinapaswa kuwapo shuleni.

Pia, kadri shuleni kunapokuwa salama dhidi ya majanga ya kijamii kama vile matukio ya moto, kunabeba maana kwamba hata maendeleo ya taaluma yatapatikana, huku wazazi na walezi wa wanafunzi husika wakiwa hawana shaka.

Kwa hatua iliyofikiwa sasa, mamlaka za kiserikali zenye dhamana na usimamizi na maslahi ya umma kwa upande wa shuleni, zikiwamo katika maeneo ya Elimu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, zinapaswa kuliangalia hilo kwa mapana.

Matukio ya moto yanaonekana kuwa na mwenendo endelevu, hivyo kuna kila sababu ya hatua kuchukuliwa kupata jibu la kina kuhusu chanzo, ili hali hiyo ikomeshwe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Watakaofeli kidato cha sita watazamwe

Na Mwandishi Wetu

MITIHANI ya kidato cha sita imekamilika wiki iliyopita baada ya serikali kuwaruhusu wanafunzi kurejea tena darasani miezi mitatu baada ya likizo ya corona iliyoanza Machi 17, 2020.

Miezi mitatu kukaa nje ya darasa si kazi ndogo na kuna uwezekano wa wanafunzi wengi kushindwa kufanya vizuri kwenye mitihani hiyo. Hatuliombei hilo lakini, ni jambo la kutazamwa kwa jicho la pili.

Mitihani iliyomalizika inayoandaliwa na Baraza la Taifa la Mtihani (NECTA), licha ya kulenga kupima uelewa, ujuzi na stadi mwanafunzi alizopata baada ya kukaa darasani kwa kipindi cha miaka miwili, imefanyika wakati ambao wanafunzi 'walivurugwa'.

Walitatizwa na corona kutoka na ukweli kuwa hata kusoma wakiwa nyumbani ilikuwa ni jambo gumu.

Haikuwa rahisi kwa wengi kutulia nyumbani na kusoma, lakini serikali ilipiga marufuku masomo ya ziada na mikusanyiko ambayo ingetishia maisha ya wanafunzi hao.

Watoto hao walishindwa kujifunza kwa dhati na huenda walikwamishwa na kutokujua hatima ya masomo kwa vile hawakufahamu ni lini wangerejea tena shuleni.

Kwa kawaida kiwango cha uelewa na hata ufaulu hutofautiana kutoka mwanafunzi mmoja na mwingine, jambo linalochangiwa na mambo mengi yakiwamo ya kimaumbile, mazingira ya shuleni na ya nyumbani pamoja na fursa zilizopo.

Wengi wanaamini kuwa uwezo wa akili unaweza kuwa ni urithi mtu anaopata kutoka kwa wazazi wake, mazingira anayosoma kama uwepo wa walimu, upatikanaji wa vifaa vya kufundishia, ikiwamo vitabu, maabara na utaalamu.

Walimu wa kutosha waliona ujuzi na morali wa kufundisha inaweza kuwa kati ya sababu ya mwanafunzi kufanya vizuri.

Nafasi mfano, muda wa kutosha wa kujisomea, kujumuika na wenzake kufanya mijadala ili kuongeza uelewa baada ya muda wa masomo wa darasani yote hayo husaidia kufaulu. Kupewa kazi nyingi hasa mabinti badala ya kusoma kunaweza kuchangia kuwakwamisha kufaulu.

Inawezekana wakati wa corona wengi hawakupata nafasi ya kutosha ya kujisomea na pia walichanganyikiwa kutokana na mambo yalivyokuwa hasa hofu, hivyo huenda wakapata alama za chini.

Kutokufaulu kunamaanisha kuwa inawezekana wakaachwa kwenye nafasi za vyuo vikuu hasa kupata mikopo ya elimu ya juu.

Changamoto hii haiwahusu wanafunzi ambao wazazi na walezi wao wanao uwezo wa kuwalipia na kuwapeleka popote kwa ajili ya masomo ya vyuo vya elimu ya juu.

Kuna wasiwasi kuwa huenda mabinti wakafeli kutokana na ugumu wa maisha ya mazingira yanayowazunguka. Kwa hiyo ingekuwa vyema kama watakaokosa fursa wakasaidiwa wasiachwe kupoteza kila kitu kutokana na changamoto za maisha waliyokutana nayo wakati wa corona.

Ni vyema mabinti ambao mara nyingi huwa waathirika wakapata mbadala wa kuwasaidia hata kama watakuwa wamefeli kwenye masomo ili kujiendeleza kwa kuwa corona imekuwa na athari nyingi kielimu.

Kufikiria suala mbadala kwa wasichana ni jambo jema kwa kuwa corona ilisababisha wanafunzi kukaa nyumbani miezi mitatu ambao ni muda mrefu.

Ikumbukwe kuwa kufeli mtihani kunaweza kuwa na sababu nyingi, pengine wakati huo, mwanafunzi hakuwa sawa kisaikolojia kutokana na yaliyomfika wakati wa likizo ya corona. Wapo walionyanyaswa kijinsia, kuna waliopewa mimba na wakati mwingine kutumikishwa kazi kupindukia hasa vijijini na watoto wanaotoka katika familia maskini.

Kwa hiyo, serikali, wadau na watetezi wa haki ya mtoto kuna haja ya kuanza kutafakari jinsi ya kuwasaidia wanafunzi watakaofeli kwenye matokeo ya mtihani wa kidato cha sita kwa kuwa ulifanyika katika mazingira ya changamoto.

Kuwa na namna ya kuwasaidia wanafunzi hakumaanishi kuwa kila atayeanguka, anahusika sivyo. Msaada uwahusu wale waliokuwa na maendeleo ya juu na jitihada kubwa lakini 'wakavurunda' kutokana na baadhi ya changamoto ambazo hazikukwepeka.

Msaada huo unaweza kuwa fursa ya kuwawezesha kujipanga tena na kufanya vizuri katika masomo yao na wanafunzi.

# HABARI PICHANI



Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mussa Azzan Zungu, akipiga kura kuomba ridhaa ya kuteuliwa kugombea ubunge wa Jimbo la Ilala kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Ilemela, Angelina Mabula, akiwa na wagombea wenzake katika mkutano mkuu wa CCM Wilaya ya Ilemela, mkoani Mwanza jana, wakisubiri kupigiwa kura za maoni za ubunge wa jimbo hilo. **PICHA: ROSE JACOB**



Msimamizi wa uchaguzi wa kura za maoni Jimbo la Mbogwe ambaye ni Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Geita, David Azalia, akihesabu kura za maoni za kumpitisha mgombea wa jimbo hilo, jana. Kulia kwake ni Katibu wa CCM wa Wilaya hiyo, Grace Shindika. **PICHA: SHABAN NJIA**



Mfanyabiashara maarufu mkoani Arusha, Philemon Mollel, akiomba kura ya kugombea ubunge wa Jimbo la Arusha Mjini kwa wajumbe wa mkutano mkuu wa CCM Wilaya ya Arusha Mjini jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**



Baadhi ya wajumbe wa mkutano mkuu wa Jimbo la Arusha Mjini, wakisikiliza wagombea wa ubunge jimbo hilo, kabla ya kupiga kura za maoni jana. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**



Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Wilaya ya Ilala, wakipiga kura za maoni kuchagua mgombea ubunge, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

UCHAGUZI MKUU 2020

# HABARI PICHANI



Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akipiga kura ya maoni kuchagua wajumbe wa uwakilishi, ubunge katika mkutano wa Jimbo la Tunguu, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja jana. **PICHA: IKULU**



Mkurugenzi wa Udhibiti na Utawala wa Kampuni ya SportPesa, Abbas Tarimba (wa pili kulia), akipongezwa na wagombea wenzake wa kuwani nafasi ya uteuzi kugombea ubunge kwa tiketi ya CCM, Jimbo la Kinondoni, jijini Dar es Salaam, baada ya kuongoza katika kura za maoni, jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, akiwapungia mkono wajumbe wa mkutano mkuu wa CCM Jimbo la Arumeru Magharibi, wakati wa kura za maoni jijini Arusha, jana. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**



Kura za maoni za kupitisha mgombea wa CCM zikihesabiwa jana, katika Jimbo la Busenga, Mkoa wa Simiyu. **PICHA: HAPPY SEVERINE**



Wagombea wa CCM kwa ajili ya uteuzi wa kugombea ubunge Jimbo la Mbeya Mjini, wakiwa kwenye picha ya pamoja, baada ya kumalizika kwa kura za maoni, Dk. Tulia Ackson aliongoza kwa kura 834 kati ya kura 924 zilizopigwa. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**



Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson akiwa mwenye furaha, huku akiwa ameinamia rundo la kura alizopigiwa, wakati wa kuhesabu kura za maoni Jimbo la Mbeya Mjini jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

HABARI KITAIFA

# RC aingilia kati mgogoro wa ardhi Mhenda

Na Frank Kaundula, MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Loata ole Sanare, amelazimika kuingilia kati mgogoro wa ardhi uliodumu kwa zaidi ya miaka 14 katika shamba la Mhenda, lenye ukubwa wa hekari 623 baada ya wananchi wa kijiji cha Mhenda, wilayani Kilosa kulalamikia kutishiwa silaha za moto na mwekezaji akiwataka kuondoka katika eneo hilo.

Wakitoa malalamiko yao mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro wakati wa mkutano maalum wa kijiji hicho, wananchi hao walidai kuwa shughuli za kimaendeleo kijijini hapo zimesimama kutokana na mgogoro huo kwa kuwa asilimia kubwa ya wananchi ni wakulima.

Abdalah Kamwinyo, ambaye ni Kaimu Mwenyekiti wa kijiji hicho, alidai kuwa katika kipindi cha hivi karibuni wamekuwa wakitishiwa amani kwa kutishiwa bastola na mwekezaji huyo akiwataka kuondoka katika shamba hilo.

"Tunaishi kwa mashaka, juzi juzi tu hapa wajumbe wa serikali ya kijiji tumeshikiwa bastola tunaambiwa tuhame na wananchi wetu, tunashindwa kuelewa mamlaka hayo anayatoa wapi wakati tunajua Tanzania ni nchi ya amani," alilalamika Kamwinyo.

**Sisi tupo kama wamekuvamia kweli sio kuwatolea silaha, nataka hiyo bastola uisalimishe hapa na ufuate utaratibu, lakini nanyi wananchi asitokee mtu akaongeza hata sehemu kutoka eneo analolimiliki.**

Naye Fabian Mapunda, alidai licha ya mgogoro huo kudumu kwa kipindi kirefu hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwamo kufikisha sakata hilo serikali ya kata na wilaya bila mafanikio na kuwaacha wakiendelea kuishi katika hali ya sintofahamu.

"Tangu 1975 tunalima shamba hili, lakini kufikia mwaka 2006 ndipo huyu mwekezaji akaibuka na kudai kuwa eneo hilo ni la kwake, kila tukifuatilia wilayani tunazungushwa na huku kijijini tunashikiwa silaha tuondoke," alidai Mapunda.

Alipotakiwa kujibu tuhuma za kutishia watu silaha za moto, mwekezaji huyo aliyejitambulisha kwa jina Salehe Gaidi, alikana kuhusika na tuhuma hizo na kudai kuwa ni hila zinazotumiwa na wanakijiji hao ili kumnyima haki yake.

"Mimi sijawatishia silaha ninachotaka waondoke katika shamba langu ambalo lilinunuliwa na marehemu baba yangu tangu 2006 baada ya kesi kuisha, lakini wanakijiji wamekaidi tangu wakati huo hawataki kutoka na serikali ya kijiji inawakodishia watu wengine shamba hili," alidai Gaidi.

Mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama Mkoa wa Morogoro, Sanare alimtaka mwekezaji huyo kusalimisha silaha yake kwenye vyombo vya dola haraka iwezekanavyo wakati mgogoro huo ukiendelea kushughulikiwa.

"Sisi tupo kama wamekuvamia kweli sio kuwatolea silaha, nataka hiyo bastola uisalimishe hapa na ufuate utaratibu, lakini nanyi wananchi asitokee mtu akaongeza hata sehemu kutoka eneo analolimiliki," alisema.

Sanare alisema Rais John Magufuli tayari alishatoa mwongozo wa kushughulikia migogoro hiyo kwa kuunda kamati maalumu itakayoongozwa na Waziri wa Ardhi, hivyo wananchi wanatakiwa kuwa na subira wakati kamati hiyo ambayo Mkuu wa mkoa ni mjumbe, inafanyia kazi mgogoro huo.

## Bil. 3/- kujenga barabara ya Bigwa - Kisaki

Na Frank Kaundula, MOROGORO

SERIKALI imesema imetenga shilingi bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Bigwa Manispaa ya Morogoro hadi Kisaki Wilaya ya Morogoro kwa kiwango cha lami ili kuwarahisishia wakulima kusafirisha mazao yao kwenda sokoni.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Kilimo, Omar Mgumba, ambapo alieleza kuwa kukamilika kwa barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 151, kutafungua fursa nyingi za kibiashara katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo hususani Kisaki.

"Tumetenga kiasi cha shilingi bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa barabara, na kukamilika kwa barabara hii kutafungua fursa nyingi za kibiashara kwani kutamaliza changamoto ya usafirishaji wa mazao ya wakulima," alisema Mgumba.

Alisema kwa muda mrefu wakulima wamekuwa wakipaza sauti zao juu ya changamoto inayowapata wakati wa kusafirisha mazao kuyatoa Kisaki kuyapeleka Morogoro mjini na mikoa ya jirani na sasa serikali imesikia sauti hizo.

Mgumba alisema katika maeneo ya Wilaya ya Morogoro kama Kisaki, Changarawe, Mvua na kwingineko ni maarufu kwa uzalishaji wa mazao mbalimbali, hivyo kukamilika kwa barabara kutawanufaisha wakulima wengi.

"Wakati wa mvua za masika mazao mengi uharibika njiani kwani magari hukwama kutokana kuna ubovu wa barabara na kuwapa hasara wakulima, hivyo ujenzi wa barabara hii utawarahisishia usafirishaji mazao," alisema Mgumba.

Alisema barabara ya Bigwa Kisaki yenye urefu wa kilomita 151 ndiyo barabara pekee inayotumiwa na wakulima wengi wilayani Morogoro kusafirishia mazao yao kupeleka katika masoko mbalimbali nchini na nje ya nchi.

Alieleza kutokana na umhimu wa barabara hiyo, itakapokamilika inachangia kwa kiasi kikubwa kuongeza mapato ya ndani ya halmashauri hiyo na pia pato la taifa litaongeza kupitia sekta ya kilimo cha mazao yanayozalishwa na wilaya hiyo.

Kwa upande wao, wakulima wa mazao ambapo pia ni washafirishaji wa mazao kwenda kwa wanunuzi waliipongeza serikali kwa hatua hiyo ambayo imekuwa changamoto ya muda mrefu kwani itasaidia kuimarisha usafiri wa bidhaa zao.



Wananchi wakipita kwenye daraja la muda mpakani mwa Tandale na Kijitonyama, eneo la Kwa Ali Maua, jijini Dar es Salaaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Vikundi matatani kushindwa kulipa mikopo

Na Shaban Njia, KAHAMA

HALMASHAURI ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, imevifikisha mahakamani vikundi vya ujasiriamali 35 vijana na wanawake kwa kushindwa kulipa mikopo yenye riba nafuu waliokopesha na halmashauri hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu ya fedha kuanzia 2016/17 hadi 2019/2020.

Anderson Msumba, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, aliyabainisha hayo alipokuwa akizungumza na Nipashe na kushangazwa na kitendo cha vikundi hivyo kushindwa kulipa wakati vyama vingine vinaikosa.

Alisema kati ya vikundi 35 vya ujasiriamali vijana na wanawake, vikundi vitano pekee ndivyo vilivyoweza kulipa mikopo hiyo na vikundi hivyo vinavyodaiwa havitaweza kukopeshwa kwa mara nyingine na halmashauri kutokana na kushindwa kulipa madeni kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017 hadi mwaka 2018.

Msumba alitaja vikundi vilivyolipa mikopo yenye riba na nafuu na kuvipatia fursa vikundi vingine kuendelea kukopesheka na halmashauri kuwa ni kikundi cha Stendi Tunaweza, Upendo Nyahanga, Uaridi, Upendo wa Mungu na Ebeneza Nyihogo.

"Tulivikopesha vikundi 35 vya ujasiriamali, vijana na wanawake mikopo yenye riba nafuu kwa kipindi cha miaka mitatu ya fedha 2016/2017 na 2018, lengo la mikopo hiyo ni kuviinua kimitaji na kuwaondolea adha ya riba kubwa kwenye taasisi za kifedha," alisema Msumba.

Msumba aliongeza: "Kati ya vikundi 35 tulivyovikopesha mpaka sasa vikundi vitano vimekwishalipa mikopo inayodaiwa na kwa kikundi ambacho kinadaiwa na kimefikishwa mahakamani hakitaweza kukopesheka tena kutokana na kukosa sifa kwa kipindi chote hiki."

Aidha, Msumba alisema kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, halmashauri imetenga kiasi cha Sh. milioni 900 kutoka kwenye mapato yake ya ndani kwa ajili ya vikundi vya ujasiriamali vijana, kinamama na walemavu kutoka kata 20 za halmashauri hiyo.

Alisema mwaka wa fedha 2018/19 halmashauri ilitenga na kutoa shilingi milioni 564.5 na kutoa mikopo kwa vikundi 158 vya wajasiriamali vijana, wanawake na walemavu.

Pia alisema mwaka wa fedha wa 2019/20, halmashauri ilitenga shilingi milioni 618 na kutoa shilingi milioni 199 kwa vikundi vya wajasiriamali 68, robo ya kwanza ya mwaka vikundi vya kinamama 53 vilipata shilingi milioni 160 na vijana vikundi 15 vilipata milioni 39.

# Machinga wasiokuwa na vitambulisho kusakwa

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

SERIKALI wilayani Bukoba mkoani Kagera, imesema itaanza kufanya msako kwa wafanyabiashara wadogo maarufu kama wamachinga ambao wanaendelea kufanya biashara, huku wakikaidi kuchukua vitambulisho vya wajasiriamali wadogo.

Akizungumza na baadhi ya wakazi wa mitaa ya Bunkango na Bushaga katika Manispaa ya Bukoba, Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Kadole Kilugala, aliwataka wafanyabiashara hao kuchukua vitambulisho hivyo kwa hiari, kwa kuwa kwa sasa vipo vya kutosha katika ofisi za watendaji wa mitaa na kata.

**Usisubiri tuje tukufuate maana tutaanza kufanya operesheni kwa ajili ya wafanyabiashara wote wadogo ambao hawana vitambulisho.**

"Wale wafanyabiashara wadogo yaani wamachinga, tafadhari sana vitambulisho vya awamu ya pili vipo tayari, twende tukachukue kwa hiari, vinapatikana kwa Sh. 20,000 tu," alisema na kuendelea:

"Usisubiri tuje tukufuate maana tutaanza kufanya operesheni kwa ajili ya wafanyabiashara wote wadogo ambao hawana vitambulisho."

Alisema ameshasikia kuwa hata wasipochukua vitambulisho hakuna hatua zozote watakazochukuliwa, na kuwataka kutambua kuwa adhabu yake ipo, tena ni ya kisheria kwa kuwa imepitishwa na Bunge.

"Usipochukua hicho kitambulisho adhabu yake ni faini ya kuanzia shilingi 30,000 mpaka 50,000, ama kifungo kisichozidi mwaka mmoja," alisema.

Mmoja wa wamachinga waliozungumza na Nipashe kuhusiana na agizo hilo, Muddy Amri, alisema kuwa hawajagoma kuchukua vitambulisho hivyo na kuwa mwitikio mdogo unatokana na hali ngumu ya kiuchumi iliyosababisha baadhi yao kukimbia biashara.

"Kuna vibanda vimefungwa kwa sasa, sio kwamba wahusika wamesafiri bali wamekimbia biashara imekuwa ngumu, wengine tunachukua mzigo mipakani kule tunatakiwa kulipa wakati tuna vitambulisho, tunaomba serikali itusaidie kutupunguzia changamoto hizi ili kuepuka watu kukimbia biashara," alisema.

Faustine Agustine, aliomba vitambulisho hivyo vifanyiwe maboresho kwa kuwekewa picha, ili kuepuka tatizo la kitambulisho kimoja kutumiwa na mtu zaidi ya mmoja.

# Mradi wa Halmashauri Mji Nzega wamkuna RC

**Na Tiganya Vincent,** NZEGA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, ameipongeza Halmashauri ya Mji wa Nzega kwa mradi wake wa kushirikisha wananchi kupanga na kupima maeneo ili kuepuka makazi holela.

Amesema hatua hiyo imesaidia kuongeza chanzo kipya cha mapato ambacho kinatokana na uuzaji wa viwanja katika eneo la Ipazi.

Dk. Sengati alitoa kauli hiyo jana wakati wa ziara ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo. Alisema upangaji wa Mji wa Ipaza kwa kushirikisha jamii utasaidia kutatua migogoro ya ardhi na kudhibiti ujenzi holela na kuwa na mji uliopangika.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Nzega, Philemon Magesa, alisema kuwa awali walifanya majaribio kubuni mradi wa kupanga na kupima viwanja katika eneo la Idalu kwa kushirikisha jamii na kupata mafanikio.

Alisema kupitia mafanikio ya upimaji katika eneo la Idalu kwa kutumia wataalamu wake walibuni mradi mkubwa wa upimaji viwanja katika eneo la Ipazi ili kuwa na mji wa kisasa katika eneo hilo.

Alisema wananchi wa eneo hilo wameshiriki kwa asilimia 100 kuanzia mwanzo hadi mwisho wa mradi huo. Mkurugenzi huyo Mtendaji alisema katika makubaliano wananchi wanachukua asilimia 70 na halmashauri inabaki na asilimia 30 ya viwanja kama gharama ya upangaji na upimaji.

Magesa alisema halmashauri ilitumia kiasi cha Sh. milioni 273.8 ya mapato yake ndani kulipa fidia wananchi 57, ambao maeneo yao yalitwaliwa ili kutekeleza mradi huo.

Aliongeza kuwa kiasi cha shilingi milioni 50 kilitumika kwa ajili ya kupanga, kupima, kutengeneza na kupanga vigingi na kuchonga barabara na kulipa vibarua. Magesa alisema kutokana na zoezi hilo, halmashauri inatarajia kupata kiasi cha Sh. bilioni 1.2 kutokana na mauzo ya viwanja 1,606.

Alisema mpango wao ni kuendelea kupanga na kupima maeneo mbalimbali ili halmashauri hiyo iwe na maeneo ambayo yamejengwa vizuri na kisasa.



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, akishiriki ujenzi wa jengo la ofisi ya Halmashauri ya Mji wa Nzega jana, akiwa katika ziara ya kukagua shughuli za maendeleo. **PICHA: TIGANYA VINCENT**

# Ikunji yapelekewa kituo cha afya

**Na Dotto Mwaibale,** SINGIDA

MKUU wa Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, Edward Mpogolo, amewataka wajawazito katika Kata ya Iyumbu kujenga tabia ya kuhudhuria kliniki baada ya kusogezewa kituo cha afya.

Mpogolo alitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki wakati akipokea vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 5 vilivyotolewa na Benki ya NMB kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Kata ya Iyumbu.

"Kinamama sasa mmesogezewa huduma za afya na leo Benki ya NMB imewaletea msaada wa vifaa tiba, jengeni mazoea ya kwenda kliniki ili kufanyiwa uchunguzi wa afya zenu mnapokuwa wajawazito," alisema Mpogolo.

Alisema nchini kuna benki zaidi ya 49 zikiwapo na ndani ya Mkoa wa Singida, lakini ni benki ya NMB pekee ndio imeonyesha upendo na kuwa pamoja nao kwa kuwapelekea vifaa tiba hivyo.

Mpogolo alisema benki hiyo sio kwamba ina fedha nyingi, lakini imewapelekea msaada huo pamoja na madawati ya kukalia wanafunzi wa Shule ya Msingi Ntuntu yenye thamani ya Sh. milioni 5 jumla ikiwa ni Sh. milioni 10.

Alisema benki hiyo hata katika kipindi cha ugonjwa wa Covid-19 ilitoa msaada na pia serikali ilipotaka gawio kwa ajili ya shughuli za maendeleo, ilitoa zaidi ya Sh. bilioni 10.

"Niishukuru sana Benki ya NMB kwa kuunga mkono jitihada za Rais John Magufuli za kuwaletea maendeleo wananchi," alisema Mpogolo.

Aidha, Mpogolo alisema katika kipindi kifupi ambacho Rais Magufuli amekuwa madarakani, amejenga zaidi ya hospitali 67, vituo vya afya na zahanati zaidi ya 400 na kwa Wilaya ya Ikungi wamepata vituo vya afya viwili cha Kata ya Ihanja kilichojengwa kwa Sh. milioni 500 pamoja na vifaa tiba vya zaidi ya Sh. milioni 300 na kituo cha afya cha Kata ya Sepuka cha Sh. milioni 400 pamoja na vifaa tiba vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 200.

Meneja wa benki hiyo Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, akikabidhi msaada huo alisema benki hiyo wakati wote imekuwa ikisaidia shughuli za maendeleo nchini ikiwa ni kuunga jitihada za Rais Magufuli za kuiletea nchi maendeleo.

Alisema benki hiyo ina matawi zaidi ya 230 nchi nzima, lakini katika Kanda ya Kati wana matawi takribani 25 na kumwagiza Meneja wa Benki hiyo Wilaya ya Ikungi, Osward Kayuni, kuhakikisha anapata wakala katika Kata ya Iyumbu ili kuwapunguzia wananchi tatizo la kutunza fedha zao.

Nipashe
TESA
Jumanne Julai 21, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14
**Teknolojia ni fursa uchaguzi 2020**



Ukurasa 13
Bajeti maji 2021 uelekeo uwe kukata kiu shule nyingi zaidi



Ukurasa 12
**Ni maswali lukuki usahihi takwimu za corona Afrika**

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Tasnia habari inavyosuka upya kuukabili umaskini



Kutumia kompyuta kiusajisiriamali kama kurekodi matukio na habari kwenye jamii ni fursa za wahitimu wa taasisi za habari kujiajiri. **PICHA MTANDAO**

KATIKA mataifa yaliyoendelea ikiwamo Marekani, wanahabari wanapewa umuhimu wa kipekee wakiitwa muhimili wa nne wa dola.

Dola lenye mihimili mitatu ambayo ni Serikali, Mahakama na Bunge halikamiliki bila tasnia ya habari inayokusanya, kuchambua na kusambaza taarifa kutoka mihimili hiyo na maeneo mengine mengi na kuufikishia umma. Huko ndiko kunakomfanya mwanahabari kuwa sehemu ya dola.

Licha ya tasnia hiyo kuathiriwa na sayansi na teknolojia, kuhabarisha na kutumia mapinduzi ya kidijitali yaliyoibuka sasa ni eneo linaloelezwa kuwa linaweza kuwapa kipato vijana wengi kwa kujiajiri na kuajiriwa ili kuendesha maisha yao.

Ili kufanikisha azma hiyo Baraza la Taifa la Vyuo vya Ufundi (NACTE), limeboresha mtaala wa uandishi wa habari kwa ngazi za cheti, stashahada na shahada kwa lengo la kuzalisha wanahabari bora na wanaokubalika na kisoko na wanaokwenda na wakati.

Kazi ya kuuhuisha mtaala huo inawakutanisha wanaandaa mitaala wa NACTE, wanahabari, wahadhiri vyuoni na wadau mbalimbali hivi karibuni jijini Dar es Salaam, kuuhuisha.

Kwa mujibu wa NACTE kila baada ya miaka mitano mtaala huhuishwa kulingana na mazingira na kwamba lilifanya utafiti mwaka 2020 kujua changamoto za kuuboresha.

"Tulitafuta maoni kutoka kwa wanahabari, waajiri, wahadhiri, wasomaji na wana jamii. Matokeo, wengi walitaka kufundisha mbinu za kisasa za kusaka na kuandaa habari, kuhoji kikamilifu na kuibua taarifa, masuala ya uandishi wa mitandaoni na kuwa na wasomi wenye uzoefu wanaoupata kwenye kufanyakazi kwa vitendo." Ripoti ya utafiti wa NACTE inasema.

Aidha, inasema imebaini zama hizi wahitimu wa shahada za uandishi wa habari wanaohitajika na jamii ni wale wenye uadilifu, ujasiri, umahiri wa lugha na mawasiliano na wenye mbinu bora za kuchambua na kuuliza maswali kijanja ili kupata taarifa za uhakika.

Kadhalika, wanatakiwa pia wenye kufahamu sheria mfano ile ya huduma ya habari, uhalifu mitandaoni, takwimu na kanuni zake na jinsi zinavyohusika na kazi zao, ripoti inasema.

Aidha, wafahamu pia miiko ya kazi na kuheshimu haki za binadamu katika utendaji. Wawe mahiri kwenye stadi mbalimbali (multi skills) kwenye uandishi, utafiti, uongozi na utawala lakini ufasaha wa Kiswahili na Kiingereza.

"Utafiti ulibaini kuwa mbinu za utafutaji na ujasiriamali, masoko na uandishi wa makala maalumu za redio na runinga ni stadi za muhimu zama hizi kwa wananhabari zinazohitajika na soko la ajira na walaji wengine wa bidhaa za tasnia ya habari," inaongeza.

**KUONDOA UMASKINI**

Lengo la kuhuisha mtaala ni pamoja na kuutumia kuzalisha wanafunzi wanaohitajika kwenye soko na wanaoendana na mabadiliko ya teknolojia, anasema Eufrasia Matias, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Tumaini Kampasi ya Dar es Salaam, (Tudarco).

Akiwa miongoni mwa wadau wa kuuboresha, anasema miaka iliyopita hakukuwa na uandishi wala usambazaji habari wa mitandaoni.

"Vyombo vya habari vilivyokuwa vinafahamika zaidi ni magazeti, redio, runinga na barua pepe. Lakini lao jukwaa limebadilika kuna WhasApp, Twitter, Instagram na Face book'. Yanahitajika mabadiliko ili kuwafundisha vijana uandishi wa mitandaoni na namna bora kufanyakazi kidijitali na kutumia vifaa vya kielektroniki." Anasema.

Anasema kuboresha kunaondoa umaskini kwa mfano, hatua ya kwanza au 'level one' inawawezesha wanafunzi wa kidato cha nne kupata taalamu kiwango cha cheti inayowawezesha kuwa watafutaji, wabunifu wanaoweza kujiajiri kwa kuandika na kusambaza habari kwenye vyombo mbalimbali popote walipo.

"Anaweza kuwa mwanahabari wa kujitegemea anayepiga na kuuza picha, kuandika na kusambaza habari mbalimbali," anasema.

Aidha, anaweza kumiliki studio ya kupiga na kusafisha picha za kidijitali, kijijini au mjini, pia kutumia kompyuta kurekodi na kuuza nyimbo za aina mbalimbali, anasema.

"Anajiajiri kwa kupiga picha na kurekodi matukio ya sherehe na msiba. Anaweza pia kupiga picha za mikutano ya serikali za mitaa, vijijini na kusambaza taarifa kazi inayoweza kumwongozea mapato." Anasema.

**FURSA KWA WANAWAKE**

Eufrasia anaamini kuwa ni ujuzi unaoweza kutumiwa kuzungumzia changamoto za wanawake, watoto na wahitaji vijijini ambao shida zao hazijafahamika kutokana na ukosefu wa vyombo vya habari.

Anaamini kuwa kuwapo kwa elimu hiyo ya vyuo vya stadi za ufundi vinawezesha wanawake kuendelea kusoma kwa vile anaweza kumaliza cheti, akaendelea kwenye stashahada (diploma) na kumalizia shahada.

"Elimu hii ni tofauti na ile kidato cha nne na sita ambayo mwanamke akimaliza na akapata changamoto inakuwa vigumu kujiendeleza," anasema.

**ANGALIZO ULEMAVU**

Elgius Bwaliya, Mratibu wa Maendeleo ya Mitaala, NACTE, akizungumzia mtaala huo, anashauri mitaala iangalie mahitaji ya watu wenye ulemavu.

Anasema ameuchambua na kubaini kuwa licha ya kuwa na maudhui mujarabu, changamoto yake ni kukosa vifaa vya kuwasaidia wenye ulemavu kunufaika.

Anataja simu janja, vinasa sauti na zana za kujifunzia hazijazingatia mahitaji ya wenye uhitaji maalumu, mfano wasioona au kusikia.

"Wenye ulemavu hasa wa kuona wanahitaji vifaa mfano 'software ya gold wave' wanayoitumia kuhariri na kusanifu kurasa au maandiko kwenye kompyuta. Yote hayapo kwenye mtaala huu, mwanafunzi mwenye ulemavu kama asiyeona atanufaikaje" anahoji Bwaliya.

Anasema si changamoto hiyo pekee amegundua kuwa 'apps' au application za watu wasiiona wala kusikia kwenye simu ambazo ni miongoni mwa vifaa ambavyo vinavyohitajika na mtaala ili kufunza wahitaji namna ya kuvitumia ili kufikia lengo hilo.

"Kwa ujumla mtaala haujazingatia kikamilifu wenye mahitaji maalumu." Anasema Bwaliya ambaye ni mwalimu wa lugha na kushauri wahitaji kupewa kipaumbele.

SAYANSI

NA MICHAEL ENEZA

# Ni maswali lukuki usahihi takwimu za corona Afrika

## • Mshangao Marekani kulumbania barakoa



Wauguzi na madaktari wakijipanga kuwahudumia waathirika wa corona. Afrika Kusini ni nchi pekee barani Afrika yenye idadi kubwa ya wagonjwa wa maradhi hayo. **PICHA MTANDAO**

HALI ya sekta za afya katika nchi kadhaa za Afrika inaanza kutatizwa na changamoto zinazoletwa na kuongezeka kwa wagonjwa na maambukizi ya janga la COVID-19.

Inakuwa mbaya katika mazingira ya kimataifa na imeonekana Bara la Amerika Kusini na sasa Afrika Kusini ni kama inaingia katika hatari ya kukwama kwa hospitali kumudu wagonjwa na vifo vinavyotokana na COVID- 19.

Wakati vifaa tiba na hata maslahi ya kuwezesha madaktari na wauguzi kufanya kazi muda mwingi wa ziada havitoshi, idadi ya wagonjwa imeongezeka. Hali hospitalini haziridhishi na kuna wakati mgumu na mazingira mabaya zaidi.

Takwimu za mashirika ya habari na vyanzo tofauti zinaonyesha kuwa Afrika Kusini, Misri na Nigeria ambazo zina uchumi mkubwa kuliko maeneo mengine ndiyo wenye maambukizi makubwa zaidi ya virusi vya corona barani Afrika.

Katika masuala ya uwezo wa hospitali kumudu wagonjwa, hali mbaya zaidi ilielekea kuwani Afrika Kusini kabla ya maeneo mengine, ingawa katika Afrika Mashariki hali ya Uganda pia ilikuwa inaleta wasiwasi.

> Yako maeneo mengine hasa yenye mazingira ya kivita ambako mapambano dhidi ya gonjwa la corona yamekuwa kitendawili, kama Afghanistan, Syria na hata Saudia ambako idadi ya wagonjwa inaongezeka na uchumi unaotegemea...

Kuna wakati baadhi ya balozi zilianza kuamini ugonjwa huo unapanuka Tanzania, lakini hali hiyo haikudhihirishwa muda uliyopita, watu wanatoka na wako salama.

Hadi kufikia mwisho wa wiki ya pili mwezi Julai Nigeria iliripotiwa kuwa na wagonjwa 34,259 na vifo 760 wakati takwimu rasmi za Uganda zilisema kuwa kuna wagonjwa 1,043 na hapakuwa na kifo chochote kutokana na corona.

Hali hiyo ni mojawapo ya vitendawili kuhusu ugonjwa huo kuwa mara kadhaa mtu anaugua ghafla anafariki na inapokuwa hivyo inakuwa hakuna tena haja ya kurudi nyuma kuangalia alikufa kwa ugonjwa gani, na kuongezea katika takwimu.

Eneo jingine la kushangaza ni jinsi wakati fulani Kenya iling'ang'ana kupima waendesha malori wa Tanzania wakifika mpakani, wakihofia maambukizi.

Ilifikia mahali ambapo Tanzania inaonekana ndiyo inasambaza virusi vya corona kwani haikuingia katika hatua ya kufungia watu ndani ili kusafisha mazingira kabla ya watu kuruhusiwa kutoka kuendelea na shughuli za kawaida. Ila hali ilivyoendelea ikaonekana wazi kuwa viwango vya maambukizi hapa nchini ni haba, licha ya vifo vya ghafla hapa na pale ambavyo katika hisia za watu kimsingi viliunganishwa na kuenea kwa virusi vya corona.

Hata nchi za ng'ambo taarifa zinasema hakuna uhakika kuwa kila kifo kinachohusishwa na corona kinatangazwa, wakati vifo vya kawaida huwa vinaunganishwa na janga hilo.

Kwingineko duniani kiwango cha maambukizi kwa siku kilikuwa kinazidi kupanda, hadi kufikia wato 230,000 maambukizi mapya kwa siku moja, kuvuka kiwango cha maambukizi mapya 228,000 wiki ya pili ya mwezi Julai.

Juhudi ziliendelea nchini Afrika Kusini kukataza mauzo ya pombe madukani na kwenye migahawa kwa sababu pombe inapunguza uwezo wa kinga za mwili kuhimili uvamizi wa virusi vya corona, au kupona haraka. Afrika Kusini ilikuwa imeanza kulegeza vizuizi vya kutembea na kufanya shughuli za kawaida, lakini ikaanza tena kuweka vizuizi baada ya kasi ya maambukizi kuongezeka.

Licha ya kuwa wataalamu wameendelea kusisitiza ulazima wa watu kubaki nyumbani kuzuia kuenea kwa kasi kwa virusi vya corona, na kulegeza masharti hayo katika maeneo mengi kumeongeza kasi ya watu kuambukizwa, jitihada ya kulegeza vizuizi ilikuwa inaendelea kote duniani.

Zipo baadhi ya nchi tajiri ambazo zinaweza kuwahakikishia watu mahitaji yao bila wao kutoka nje na kusaidia viwanda na mashirika ya huduma muhimu, lakini si zote zinaweza kutoa chakula na fedha ya kujikimu watu wakae ndani.

Halafu uchumi katika nchi za Afrika unaathiriwa zaidi na kuzuia watu ndani kuliko ng'ambo kwani kiwango chao cha kutumia njia za kielektroniki kufanya kazi ni kikubwa.

Mauzo mengi hufanyika kwa njia ya mitandao, bidhaa husambazwa na huduma hufikishwa nyumbani, na pia malipo hufanywa kimtandao.

Kwa Tanzania bila watu kutoka nje sehemu kubwa ya biashara inadoda, haina wateja.

Yako mabadiliko ya matazamio kuhusu kuenea kwa virusi vya corona katika mabara mengine kama ambavyo imekuwa Afrika Mashariki miezi miwili sasa.

Katika kipindi cha awali, Venezuela ambayo imekuwa na migongano ya nani kiongozi halali wa nchi hiyo kati ya Rais Nicholas Maduro na aliyekuwa Spika wa Bunge Juan Guidao, ilihofiwa kuwa itakuwa na janga kubwa la corona kwa sababu uchumi wake uliowekewa vikwazo na Marekani ulionekana kuparaganyika.

Ila Shirika la Utangazaji la Uingereza, BBC linasema kwa mfumo wa hospitali nchini Venezuela angalau unamudu kutibu wagonjwa waliopo.

Yako maeneo mengine hasa yenye mazingira ya kivita ambako mapambano dhidi ya gonjwa la corona yamekuwa kitendawili, kama Afghanistan, Syria na hata Saudia ambako idadi ya wagonjwa inaongezeka na uchumi unaotegemea mafuta uko taabani kutokana na mauzo, malipo kuporomoka.

Wafanyakazi wengi wa kigeni hasa kutoka barani Asia wanarudishwa makwao na huku kampuni za nchi za Magharibi zinaangalia upya shughuli zao nchini humo, kwanza kwa kukosa cha kufanya halafu kuhofia corona. Mjadala kuhusu kusaidia nchi tofauti kupambana na corona umepungua, kila nchi ipambane na hali yake.

Kilichoeleweka duniani kote ni uvaaji wa barakoa ambao katika nchi za Asia hauna mjadala, lakini Marekani bado hakijaeleweka inaishangaza dunia kwa malumbano makali na kushindwa kuamua iwapo kila jimbo watu wavae barakoa au waache.

NA SABATO KASIKA

# Bajeti maji 2021 uelekeo uwe kukata kiu shule nyingi zaidi



Baadhi ya wanafunzi wakipata huduma ya maji kwenye bomba lililopo shuleni kwao. **PICHA: MTANDAO**

LICHA ya kwamba maji ni muhimu kwa mahitaji ya wanafunzi shuleni, bado baadhi ya shule hazina huduma hiyo, hali ambayo inasababisha usumbufu kwao na wakati mwingine kulazimika kukatisha masomo.

Huduma za msingi za maji ina maana kuwa shule ina miundombinu ya maji ya kunywa na usafi kutoka kwenye chanzo cha kuaminika ikiwamo maji ya bomba, kisima, na hata maji ya mvua.

Ripoti ya utafiti ya uwapo wa maji, huduma ya kujisafisha na usafi shuleni (Wash) ya mwaka 2018 kwa shule 2,396 inaonyesha kuwa Mkoa wa Kusini Pemba visiwani Zanzibar ni wa kwanza kwa kuwa na shule nyingi zenye huduma za maji kwa asilimia 91.9.

Kwa hali hiyo, ni wazi kwamba, kuna haja ya kuongeza juhudi za kupanua huduma ya maji katika shule kwa ajili ya kuhakikisha wanafunzi wanapata huduma hiyo bila kupoteza muda wa masomo.

Ukosefu wa maji kwenye shule inasababisha wanafunzi wa kike kukumbana na changamoto ambazo wakati mwingine hulazimika kukatisha masomo, hasa kwa ajili ya usafi.

Kwa mfano, kwa mwaka mmoja, mwanafunzi awe wa kiume au wa kike, anatakiwa kuhudhuria shule kwa siku 194 na kupata vipindi 1,740 vya masomo, lakini baadhi yao wanaweza kukwama kufikia ratiba hiyo.

Wanafunzi wa kike ndiyo waathirika wakubwa katika hili, hasa kwa sababu ya hedhi na wanapokosa huduma hiyo, inaweza kuwa siyo rahisi kwao kuhudhuria kikamilifu shuleni.

**UTAFITI SHULENI**

Katika taarifa aliyowahi kuitoa kwa vyombo vya habari na Mratibu wa Huduma ya Maji, Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni, kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Mfunzo ya Ufundi, Theresia Kuwite, ilionyesha kuwapo kwa changamoto katika baadhi ya shule.

Utafiti wa mwaka 2009 wa kuangalia hali ya maji, afya na usafi wa mazingira shuleni, ukihusisha shule 2,697 katika wilaya 16, ulionyesha kuwa asilimia sita ya shule hazikuwa na vyoo.

Aidha, asilimia 11, zilikidhi vigezo vya kuwa na tundu moja la choo kwa wanafunzi 20 wa kike na tundu moja la choo kwa wanafunzi 25 wa kiume, lakini asilimia 68 ya shule zilizotembelewa hazikuwa na maji kabisa.

Kwa mujibu wa mratibu huyo, asilimia 32 ya shule zilikuwa na maji, lakini ambayo siyo ya uhakika, huku asilimia moja ya shule zikiwa hazina vifaa kwa ajili ya wanafunzi kunawia mikono.

Aidha, ripoti ya utafiti wa uwepo wa maji, huduma ya kujisafisha na usafi shuleni (Wash) ya mwaka 2018 iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) Februari mwaka huu, inaeleza kuwa asilimia 49.3 ya shule za vijijini ndizo zina huduma ya maji ikilinganishwa na asilimia 68.5 ya shule za mjini.

Kwamba, huduma za msingi za maji ina maana kuwa shule ina miundombinu ya maji ya kunywa na usafi kutoka kwenye chanzo cha kuaminika ikiwamo maji ya bomba, kisima, maji ya mvua au chupa.

Kutokana na hali hiyo, serikali ilizindua Mwongozo wa Kitaifa Kuhusu Maji, Usafi wa Mazingira kwa Shule za Msingi na Sekondari (Swash), ili kuwe na utoaji bora na ufanisi wa huduma ya maji, afya na usafi kwa wanafunzi.

Pamoja na juhudi hizo, baadhi ya shule bado zinakabiliwa na uhaba wa huduma ya maji kwa ajili ya wanafunzi, hali ambayo inawaibua wadau wa kutetea haki za wanawake ambao wanatoa wito.

> “Uchache wa wanafunzi wanawake kwenye taasisi za sekta ya maji na pia kasi ndogo ya kufikisha huduma ya majisafi na salama kwenye taasisi za elimu ya msingi na sekondari na hata katika vitu vya afya,” anasema Monica.

**MRENGO WA KIJINSIA**

Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), ambao wanajihusisha na utetezi wa haki za wanawake, unasema kuna umuhimu kwa bajeti kuzingatia mrengo wa kijinsia ili kuwapunguzia wanawake changamoto zinazowakabili kwenye maji.

Ofisa Programu Idara ya Habari wa TGNP, Monica John anasema, kuna sababu zinazochangia kuwapo kwa changamoto mbalimbali kwenye sekta ya maji nchini, ambazo zinaumiza wanawake wakiwamo wanafunzi.

Anasema kufifia kwa uzingatiaji wa usawa wa kijinsia katika kamati, bodi na mifumo ya uongozi kwenye vyombo vya sekta ya maji, vinasababisha hali hiyo na pia vyanzo vya maji kuwa zaidi ya umbali wa nusu kilometa.

“Uchache wa wanafunzi wanawake kwenye taasisi za sekta ya maji na pia kasi ndogo ya kufikisha huduma ya majisafi na salama kwenye taasisi za elimu ya msingi na sekondari na hata katika vitu vya afya,” anasema Monica.

Anaongeza kuwa hakuna mchanganuo wa kijinsi na kijinsia, hali ambayo husababisha athari za ukosefu wa huduma za majisafi na salama kwa wanawake na wasichana kwenye vijiji na miji.

“Hali hiyo inasababisha kuendelea kuwapo kwa mdondoko wa wanafunzi wa kike na wa kiume kwenye mfumo wa elimu ya msingi na hii na mengi ndiyo yanayotupa uhalali wa kudai bajeti ya kijinsia,” anasema.

Anasema sera ya maji ya mwaka 1991, inaelekeza kuwa ifikapo 2002 maji yawafikie wananchi kwenye umbali usiozidi mita 400 kwa vijijini na mita 300 kwa mijini na kwamba wenye jukumu la nyumbani ni wanawake wakiwamo wanafunzi.

“Sasa kwa mazingira kama hayo, wakati mwingine wanafunzi wanachelewa kwenda shule wakitafuta maji, hivyo suala la bajeti kuzingatia mrengo wa kijinsia ni la muhimu sana,” anasema.

**BAJETI YA MAJI 2020/2021**

Katika bajeti ya mwaka 2020/2021, Wizara ya Maji, imetenga Sh. bilioni 733,284,075, yenye lengo la kuboresha huduma hiyo muhimu kwenye jamii.

Bajeti hiyo imekuwa kubwa kuliko ile ya mwaka 2019/2020, ambayo ilikuwa ni Sh. bilioni 634,196,530, hali ambayo inaonyesha serikali imejipanga kuendelea kuimarisha na kuboresha huduma hiyo.

Pamoja na hayo, Dira ya Taifa ya Maendeleo inalenga kuboresha huduma za maji vijijini kufikia asilimia 95 ifikapo mwaka 2025 na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, serikali inatekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ya mwaka 2006 - 2025.

Hiyo ni awamu ya pili ya utekelezaji wake kwa sasa na katika uboreshaji na kuleta ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya maji vijijini, ilianzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa).

TEKNOLOJIA

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Teknolojia ni fursa uchaguzi 2020

## •SMS, WhatsApp, video kwa wagombea

KWENYE vijiji vingi Tanzania zama hizi kuna umeme na kila mahali kuna mwanga unaowawezesha kuendesha shughuli za kiuchumi, kitaaluma na kuwasiliana ili kuhabarika kupitia mitandao ya kijamii, simu, runinga na redio.

Hotuba ya Bajeti Wizara ya Nishati ya mwaka 2020/21 inathibitisha kuwa Aprili mwaka huu vijiji 9,112 vilikuwa na umeme na vilivyobakia 1,822 vitapata nishati hiyo wakati wowote.

Kuwapo kwa umeme kila mahali nchini ni fursa wakati wa uchaguzi kwa vile kunafungua milango kwa wapigakura kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHEMA) kuwasiliana na wagombea kwa ufanisi kuanzia sasa hadi muda wa uchaguzi mwezi Oktoba.

Itakumbukwa kuwa umeme huo ndiyo unaowawezesha wananchi kutumia mitandano mbalimbali ya mawasiliano kama simu, kompyuta, vituo vya redio, televisheni, intaneti, popote walipo bila kujali ni kijijini au mjini kuwasiliana.

Hivyo, hiyo ni fursa kwa wapigakura kuwasiliana na wagombea, udiwani, ubunge, uwakilishi, urais, vyama, serikali na mamlaka za kusimamia uchaguzi kuwaeleza mawazo na maoni yao kuhusu jinsi ya kuboresha maisha yao na mambo mengi ya msingi wanayotaka serikali iwafanyie kupitia mchakato huo wa kidemokrasia.


Akizungumza na Nipashe kuhusu umuhimu wa TEHAMA kwenye uchaguzi mkuu na jinsi inavyoweza kutumiwa na wapigakura kufanikisha mchakato huo wa kidemokrasia, Egerbert Mkoko, Mhadhiri wa Shule Kuu ya Uandishi wa Habari ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, (SJMC) anasema TEHAMA ni nyenzo muhimu ya mawasiliano.

Teknolojia hiyo inaweza kutumiwa kutoa maoni, kujieleza na kuwasiliana na mgombea kwa njia ya ujumbe SMS, kupiga simu, kuandika ujumbe kwenye 'WhatsApp', 'Twitter', tovuti, barua pepe au kupiga picha na kufikisha ujumbe kwa anayekusudiwa.

Zama hizi si lazima kulalamika kuwa hujafikiwa na mgombea kwenye mkutano, fursa mojawapo ya kumfikia na kutoa maoni ni kwa njia ya TEHAMA ikiwamo pia kutumia vyombo mbalimbali vya habari kama magazeti, redio na televisheni ambavyo vimefika vijijini kama ilivyo mijini, anashauri.

Anakumbusha kuwa vijijini kuna redio za kijamii. Pia mkongo wa taifa wa mawasiliano umesambaza mawasiliano ya 'internet'. Yote hayo yamewezesha kupata redio na televisheni mtandao na kwamba mitandao yote hiyo ni fursa kwa wananchi kutoa mawazo, maoni, hisia na kujieleza kwa wagombea.

Anaiona kuwa ni fursa ya kuwasiliana na serikali, vyama, wagombea na wapigakura. Aidha, kutumia haki ya kusema kila mpigakura anachotaka ili mradi havunji sheria kueleza masuala ya msingi anayotaka serikali, chama au mgombea awafanyie au atekeleze na kumweleza pia changamoto na fursa.




Simu ni nyenzo ya kuwasiliana na viongozi wakiwamo wagombea pamoja na wanajamii. **PICHA: MTANDAO**

> "Kama wapigakura wakuu wana haki ya kusikilizwa na ili ajenda zao zipate nguvu ni vyema kutumia haki ya kutoa maoni na kujieleza, lakini kushiriki kwenye kugombea na kuchaguliwa kwenye nafasi za uongozi wa kisiasa," anasema Lilian, mbobezi wa uandishi mahiri pamoja na menejimenti.

### KUTOA MAONI

Mwalimu Johnson Soah wa Chuo cha Uandishi wa Habari cha DSJ cha Dar es Salaam, anapozungumzia suala la teknolojia kurahisisha uchaguzi na utaratibu wa kutoa maoni, anasema pamoja na kutumia mifumo mbalimbali ya mawasiliano kama simu, kompyuta na tovuti wakati huu wa uchaguzi wananchi wasikae kimya kwenye mikutano ya kampeni watafute nafasi ya kueleza changamoto zao.

Anawakumbusha kuwa kipindi hiki cha uchaguzi ni wakati mufaka wa wapigakura na wananchi kueleza shida zinazowakabili na kutaja kile wanachotaka wagombea uchaguzi mkuu wakifanikishe.

"Wazungumzie mifumo, taratibu na maoni yao ili vyama, wagombea na serikali waweke kwenye ajenda za mambo ya kutekelezwa kwenye kipindi kingine cha miaka mitano ijayo," anashauri Soah.

Soah anayefundisha mbinu mbalimbali za kukusanya habari, uandishi wa makala na habari za michezo anasema wakati huu wa kuelekea kwenye kampeni ni fursa kwa wapigakura kuangalia ilani na ajenda za vyama kama zinawagusa wananchi moja kwa moja ama ni ahadi zisizowaridhisha.

Anawakumbusha wapigakura kuwa ni kipindi cha kutathmini ahadi zilizotolewa na viongozi waliomaliza miaka mitano kama hakuna mabadiliko jimboni au kwenye kata ni fursa ya kueleza maoni na kumfikisha mgombea taarifa kwa njia mbalimbali pamoja na TEHAMA.

Soah anasema teknolojia inawezesha kurekodi matukio, hali duni za wananchi na sauti mbalimbali za wagombea. Kwa hiyo ni vyema pia kutumia mbinu hiyo na kuwakumbusha na kuwahoji wanafeli wapi?

Shirika la CDHR la 1948 la Haki za Binadamu linaeleza umuhimu wa haki ya kidemokrasia ya uhuru wa kuchagua na kuchaguliwa pamoja na uhuru wa kutoa maoni yao kwenye mchakato wa kuchagua viongozi.

### USTAWI WA WANAWAKE

Wakati huu wa uchaguzi ni muhimu kwa wanawake kutumia teknolojia za mawasiliano kutoa maoni yao na kuibua hoja na kujua iwapo ilani za uchaguzi, vyama na wagombea wameweka ajenda au mikakati ya kuhakikisha ustawi wa wanawake, watoto, wenye ulemavu na mahitaji maalumu.

Mwalimu Lilian Nyingisye wa DSJ anasema na kuongeza kuwa ni muhimu kinamama kupaza sauti zao ili kuhoji kama serikali imetunga sheria zipi za kuzuia na kuadhibu ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika muhula uliopita na katika awamu ijayo inaahidi kitu gani?

"Wanawake wawahoji wagombea na kutoa maoni yao. Waangalie wamepewa fursa na vyama kugombea ubunge majimboni? Vipi wameshirikishwa kikamilifu kwenye nafasi nyingine za uongozi kitaifa, kwenye mikoa na hata kwenye kata mfano kwenye mabaraza ya ardhi," anasema.

Anawakumbusha pia kuzipitia ilani ili kufahamu iwapo kuna mambo yaliyoahidiwa ya kukomesha ukatili dhidi yao na kama kuna mikakati iliyolenga kuwawezesha na kuwapa sauti kiuchumi, kisiasa na kijamii kadhalika kuchunguza iwapo imetekelezwa.

Anasema kama hayo yanakosekana watoe maoni na kujieleza ili yawekwe kwenye ajenda za uchaguzi ili kuwaondoa kwenye giza la umaskini na unyanyasaji.

Aidha, mwalimu Lilian anawahamasisha wanawake kutoa maoni yao kwa njia mbalimbali iwe kwa teknolojia na kutumia haki ya uhuru wa kujieleza kwenye mikutano ya kampeni ikiwamo kutaka sheria za kuondoa ukatili na unyanyasaji na kusisitiza wapendekezwe kugombea nafasi mbalimbali za uongozi na vyama vyao ili kupata uwakilishi wenye usawa wa kijinsia.

"Kama wapigakura wakuu wana haki ya kusikilizwa na ili ajenda zao zipate nguvu ni vyema kutumia haki ya kutoa maoni na kujieleza, lakini kushiriki kwenye kugombea na kuchaguliwa kwenye nafasi za uongozi wa kisiasa," anasema Lilian, mbobezi wa uandishi mahiri pamoja na menejimenti.

### CHA KUFANYA

Lameck Isaya, mtaalamu wa mikakati ya kutumia mitandao kwa tija wa kampuni ya Lay Agency, anasema ni wakati wa kuwa na malengo na mbiu ya kampeni.

Anawaambia wapigakura kuwa wanaweza kutoa malalamiko yao wakayatuma kwenye akaunti au anuani ya 'Twitter, WhatsApp, Facebook au kama huna simu janja tuma SMS'.

Wanaweza kutuma matatizo ya kilimo, ajira, afya na matatizo ya wanawake kwa mgombea udiwani, ubunge, urais au chama kwa ujumla ni kutumia mitandao kuzungumzia kero za jamii.

Uchaguzi mkuu wa wabunge, madiwani, wawakilishi na rais unatarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu. Kampeni zinatarajiwa kuanza tarehe zitakapotangazwa na Tume ya Uchaguzi.





## NGONEDO yatambulisha mradi uboreshaji maji

**Na Peter Mkwavila,** BAHI

MTANDAO wa asasi za kiraia mkoa wa Dodoma (NGONEDO), umetambulisha mradi wa mapitio ya hatua zilizofikiwa na wadau pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Bahi kuhusu uboreshaji wa huduma za maji kutokana na mradi wa kujengea uwezo jamii.

Akizungumza wakati wa mkutano wa kutambulisha mradi huo mbele ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Bahi, Dk. Fatma Mganga, Mratibu wa NGONEDO, Edward Mbogo, alisema mradi huo unalenga kufanya mapitio.

Alisema lengo jingine ni kufuatilia matokeo ya utekelezaji wa miradi ya maji uliofanyika katika kata nne ili kuona mafanikio, ufanisi na changamoto zake na hatimaye kuwa na rejeo bora namna ya kutekeleza miradi ya kijamii kwa lengo la kuonyesha mrejesho chanya kwa jamii.

Vile vile, alisema mradi huo unalenga kupata rejea na kujifunza kwa maslahi ya pande zote na ni namna gani bora zaidi ya kuitekeleza miradi hiyo na jamii iweze kutoa tija bora na chanya bila kuathiri umuhimu wake kwa jamii.

Kadhalika, alisema malengo mengine mahsusi ni kujua hatua gani zimechukuliwa na wananchi pamoja na Halmashauri ya Bahi, katika kuboresha huduma za maji kwa mtazamo wa sera na Sheria ya Maji.

Mbogo alisema mradi huo utatekelezwa katika Wilaya ya Bahi kata za Bahi, Mpamantwa, Mundemu na Msisi na vijiji vikiwamo Bahi, Mkakatika, Mchito na Nguji.

Alisema mradi huo utatekelezwa kwa muda wa miezi sita kuanzia Julai 2020. Alisema walengwa wa mradi ni asasi za kiraia, jamii, wajumbe wa kamati za PETS, kutoka kata nne na vijiji vinne. Mbogo alisema gharama za mradi ni Sh. milioni 30.

Alisema matokeo tarajiwa ya mradi ni kuongezeka kwa uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa kupata taarifa za kifedha na kushiriki katika kukuza uwazi na uwajibikaji katika sekta ya maji.

Pia kuongezeka kwa uwazi na uwajibikaji wa halmashauri katika kutoa na kusambaza taarifa za mapato na matumizi katika miradi ya maji na ushiriki na ushirikishwaji kwa wananchi na asasi za kiraia katika kupanga, kutekeleza na kutathmini mpango wa utekelezaji wa shughuli za halmashauri utaongezeka.

# UDOM yatenga fungu kusaidia wanataaluma

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Ndaki ya Biashara na Sheria Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Profesa Adam Mwakalobo, amesema chuo hicho kimetenga fungu maalum kwa ajili ya kuwasaidia wanataaluma wachanga wanaochipukia katika fani mbalimbali.

Mwakalobo, alisema hayo juzi jijini Dodoma, wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufungua mafunzo ya uhuru wa kujieleza kwa wanataaluma.

Alisema, chuo kimetenga fungu maalum kwa ajili ya kuwasaidia wanataaluma wachanga wanaochipukia ili kuwajengea uwezo.

"Chuo kinawasaidia wanataaluma wachanga waweze kuomba fedha ambazo wakipata wanaenda kufanya utafiti mbalimbali kulingana na maeneo yao ingawa sio kitu kikubwa sana, lakini ni kuwawezesha ili waweze kujiendeleza, kwavsababu unajua kuandika machapisho na kwenda kushindana ni lazima uwe umejifunza namna ya kuandika andiko," alisema Profesa Mwakalobo.

**Kwa sababu kisheria ukisema uhuru wa kujieleza kuna mipaka, kuna haki, kuna vitu huwezi kusema licha ya kuwa una uhuru wa kujieleza, lakini vilevile kuna vitu unaweza ukavisema, lakini kwa mipaka fulani.**

Alisema mafunzo yatakuwa ni endelevu kwa sababu mwalimu muda wote anapaswa kupata mbinu mpya na vitu vipya kwa kuwa kila siku kumekuwa na mabadiliko mapya.

"Unajua mabadiliko yapo kila siku na kuna vitu vinaingia kwa hiyo ni lazima tupate mbinu mpya za kufundisha na kujifunza, huwezi kukaa tu muda wote, lazima upate mbinu mpya za kufundisha uongeze ujuzi kila wakati kwa sababu ya haya mabadiliko yanayoendelea ndiyo maana ya haya mafunzo," alisema.

Alisema wanataaluma wanatakiwa kuwa na uhuru wa kuchapisha kulingana na mambo wanayoyaona, machapisho ni moja kati ya vigezo vinavyotakiwa kutimizwa ili wapande vyeo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Sheria UDOM, Dk. Ines Kajiru, alisema mafunzo kama hayo yanafanyika ili kukuza uelewa na kuwasaidia wanataaluma kuwajengea uwezo katika masuala mbalimbali.

"Ni wengi wanaonufaika katika mafunzo kama haya, nitolee mfano hapa leo watakao nufaika ni walimu wanataaluma wote wa Ndaki ya Taaluma za Biashara na Sheria wa Chuo Kikuu cha Dodoma," alisema Kajiru.

Mwalimu katika shule ya sheria, Nicodemus Kusenha ambaye ni Katibu wa East African Network For University Law Clinics (EANUUALAC), alisema mafunzo hayo yanaongeza uelewa juu ya dhana ya uhuru wa kujieleza.

"Kwa sababu kisheria ukisema uhuru wa kujieleza kuna mipaka, kuna haki, kuna vitu huwezi kusema licha ya kuwa una uhuru wa kujieleza, lakini vilevile kuna vitu unaweza ukavisema, lakini kwa mipaka fulani," alisema.

"Mfano sisi Tanzania tuna Sheria ya Takwimu ambayo inazuia baadhi ya mambo kwa hiyo mafunzo kama haya yanawafundisha washiriki wajue mipaka ya uhuru wa kujieleza, lakini wajue ni yapi ambayo yanaweza yakazuiwa," alisema.

Mafunzo hayo yamefanyika kwa ushirikiano wa umoja wa vituo vinavyotoa msaada wa kisheria wa vyuo vikuu Afrika Mashariki.



Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana Wafanyabiashara Soko la Sabasaba jijini Dodoma, Dickson Msungu, akiwaonyesha waandishi wa habari hati ya usajili wa umoja wao, iliyotolewa na Halmashauri ya Jiji hilo, mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mhazini wa umoja huo, Athuman Said na (kushoto) Mwenyekiti Msaidizi, Rehema Kweka. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Vijana watakiwa kujiepusha kutumiwa na wanasiasa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

UMOJA wa vijana wa wafanyabiashara soko la Sabasaba jijini hapa, wamewataka vijana nchini kutokukubali kutumiwa na wanasiasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu, Oktoba, mwaka huu.

Wamesema hali hiyo inaweza kuwasababishia kuwachagua viongozi watakaoligharimu taifa kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Rai hiyo ilitolewa na Katibu Mkuu wa umoja huo, Dickson Msunga, alipokuwa akizungumza na waandishi habari jijini hapa.

Msungu, alisema kuwa katika kipindi hiki ni vizuri vijana wakachukua tahadhari kubwa kwa kujichunga na vitendo vya rushwa kutoka kwa wagombea ambao wanaamini wakiwatumia wanaweza kufanikiwa kupata nafasi.

Alisema vijana wengi wanatumika kama sehemu ya maganda ambayo yakishamenywa hutupwa jalalani kwa kuwa hayana kazi tena.

Pia alisema ni wajibu wa kila kijana kujilinda na viongozi hao ambao wakishachaguliwa wanaweza kuigharimu nchi hii kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

"Ninawasihi vijana wenzangu wasitumike kama maganda ambayo yakimenywa hutupwa jalalani, kwa kuwa hayana soko tena hivyo tunatakiwa kuchukua tahadhari ili tusifanye makosa ambayo yatatuumiza kwa kipindi cha miaka mitano," alisema.

Athumani Saidi, aliwataka vijana wenye vigezo vinavyotakiwa kujitokeza kwa wingi kwenye mchakato huo wa uchaguzi mkuu 2020, badala ya kuendelea kuwabebea mikoba na kuwapigia debe wengine.

"Vijana tusiwe kama wapiga debe wa kwenye stendi ambao kazi yao ni kupiga debe, lakini wao hawasafiri, kwa maana hiyo katika uchaguzi huu ninawasihi vijana wasiishie hivyo bali na wao waweze kukata tiketi ili waweze kusafiri kuwania nafasi hizo za ubunge, udiwani na uwakilishi," alisema.

Rehema Kweka, Mwenyekiti Msaidizi wa umoja wa vijana hao kwa upande wake aliwataka vijana waliojiandikisha kuhakikisha wanatumia demokrasia yao ya kupiga kura kwa kuwachagua viongozi watakaomsaidia Rais kwenye utendaji wa mwendokasi.





# Watoto, watu wazima walazwa wodi moja

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

WATOTO wanaougua na kulazwa katika Kituo cha Afya cha Mwakaleli kilichopo Kata ya Kandete, Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe katika mkoa wa Mbeya, wanachanganywa wodi moja na watu wazima kutokana na kituo hicho kutokuwa na wodi ya watoto.

Wataalamu wa afya wanadai kuwa hali hiyo inasababisha afya za watoto hao kuwa hatarini zaidi kwa kuwa wanaweza kuambukizwa magonjwa kutoka kwa wagonjwa wengine ambao ni watu wazima.

Akizungumza mbele ya Kamati ya Siasa ya Halmashauri ya Busokelo ambayo ilikuwa ikipita kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Diwani wa Kata ya Kandete, Botulya Kagenda, alisema kuwa suala hilo ni kero kubwa kwa wananchi wanaokwenda kutibiwa kwenye kituo hicho.

**Katika bajeti ya mwaka huu wa fedha, halmashauri imetenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa wodi mpya ya watoto katika kituo hicho.**

"Katika kituo hiki cha afya kuna malalamiko mengi kutoka kwa wananchi ambao wanaleta watoto wao kutibiwa, wakilazwa wanachanganywa wodi moja na watu wazima, kitu ambacho hawaridhiki nacho," alisema Kagenda.

Kagenda aliiomba serikali kusaidia mchakato wa ujenzi wa wodi mpya kwa ajili ya watoto kwa lengo la kumaliza kadhia hiyo ambayo imekuwa ya muda mrefu.

Katika hatua nyingine, mlinzi wa hospitali hiyo, Ashery Mwakyoma, alidai kuwa usalama wa wagonjwa na mali za kituo hicho cha afya ni mdogo kutokana na kutokuwapo uzio.

"Kituo hiki hakina uzio, hivyo watu wanaoingia na kutoka kila mtu anapita popote, hali hii inasababisha suala la ulinzi kuwa gumu na pia kuhatarisha usalama wa mali za kitu na wagonjwa, naomba hili pia liangaliwe na kufanyiwa kazi," alisema Mwakyoma.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Busokelo, Eston Ngilangwa, alikiri kuwapo kwa changamoto hizo na kueleza kuwa halmashauri yake imeanza kuchukua hatua za kukabiliana nazo.

Alisema katika bajeti ya mwaka huu wa fedha, halmashauri imetenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa wodi mpya ya watoto katika kituo hicho.

Hata hivyo, Ngilangwa aliwataka wananchi kutumia nguvu zao kuanza ujenzi wa wodi kwenye kituo hicho kabla ya serikali kuingiza fedha kwa lengo la kuharakisha maendeleo.

"Katika bajeti ya mwaka huu tumetenga fedha kwa ajili ya sekta ya afya ambazo pia tutazielekeza kwenye kituo hiki kwa ajili ya kutatua changamoto hizi, lakini pia wananchi wanaweza kuanza kwa kutumia nguvu zao ili kuharakisha utatuzi wa changamoto hizi," alisema Ngilangwa.

## TAKUKURU yaonya kuelekea uchaguzi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKATI harakati za vyama vya siasa kutafuta watakaoviwakilisha vyama vyao kupeperusha bendera kwenye uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani Oktoba mwaka huu, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya, imetoa tahadhari kwa wananchi kuwatochagua viongozi wala rushwa.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, Julieth Matechi, alisema wananchi wanatakiwa kuwachagua viongozi ambao wanatatua kero zao na sio kuwachagua wanaoupata uongozi kwa njia ya rushwa.

Matechi aliwataka wananchi kushirikiana na taasisi hiyo kukabiliana na vitendo vya rushwa kwa kutoa taarifa za viashiria vya vitendo hivyo pamoja na kuepuka kushiriki vitendo hivyo, ambavyo alisema kuwa ni kinyume cha sheria za nchi.

"Kipindi hiki cha uchaguzi ndio fursa ya wananchi kuwatathmini viongozi waliokuwapo madarakani kama wametatua matatizo yao na kuleta maendeleo, vilevile ni wakati sahihi wa kuchagua viongozi wasiokuwa wala rushwa," alisema Matechi.

Alisema kwa mujibu wa kifungu namba 15 cha Sheria ya TAKUKURU ya mwaka 2007, ni kosa kwa mtu yeyote kutoa ama kupokea rushwa na kwamba kitendo hicho ni kosa la jinai kwa mujibu wa sheria hiyo.

Matechi alisema taasisi hiyo inaendelea kutoa elimu kwa makundi mbalimbali kuhusu kukabiliana na tatizo la rushwa ili kila mmoja atambue madhara ya vitendo hivyo.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya (kushoto), akikagua vipando vilivyoandaliwa kwenye viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya, ambavyo vitatumika kwenye Maonesha ya Wakulima (Nanenane) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, yatakayoanza Agosti Mosi, mwaka huu. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Katibu Mkuu aagiza maandalizi Nanenane

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, amewataka wadau wote wa kilimo zikiwamo taasisi za umma na binafsi kuendelea na maandalizi ya Maonesho ya Kilimo (Nanenane) yatakayoanza Agosti mosi mwaka huu.

Maonyesho hayo yatafanyika katika kanda nane nchini ili waweze kushiriki kwa lengo la kutoa elimu, teknolojia na mbinu zitakazowasaidia wakulima kuongeza uzalishaji na kuleta tija katika sekta ya kilimo.

Kusaya aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea na kukagua maandalizi ya Uwanja wa Maonyesho ya Kilimo wa John Mwakangale jijini Mbeya, ambao hutumiwa na mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwa shughuli za maonesho ya Nanenane.

Alisema maonesho ya Nanenane yatumike kuongeza ujuzi na maarifa katika kukuza na kuongeza uzalishaji wa mazao kwa kupata elimu ya namna ya kuzalisha kwa tija.

"Nawaomba wadau wa kilimo hususani taasisi zinazohusika mjikite katika kuwasaidie wakulima kupata elimu na teknolojia ambayo itawasaidia kuongeza ujuzi na maarifa ya namna ya kuzalisha kwa tija," alisema na kuongeza:

"Tunahitaji kumsaidia mkulima apate faida katika kilimo chake na hili litafanikiwa endapo serikali na wadau wa kilimo tukiwasaidia wakulima kuwapa elimu na teknolojia ya uzalishaji."

Akizungumzia maandalizi ya uwanja huo kuelekea kwenye maonyesho ya Nanenane mwaka huu, Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya uwanja wa John Mwakangale, Hamza Mvano, alisema yanaendelea vizuri na kueleza kuwa mpangilio wa maonyesho mwaka huu umeboreshwa zaidi.

Alisema miongoni mwa maboresho ya mwaka huu ni kuhamasisha ushiriki kwa taasisi nyingi kushiriki maonyesho hayo, miundombinu ya barabara kuboreshwa pamoja na miundombinu mingine ikiwamo maji.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema taasisi hiyo imeandaa teknolojia zaidi ya 40 ambazo watawaonyesha wananchi kwenye maonyesho hayo ya Nanenane mwaka huu.

Alisema saambamba na kuandaa teknolojia hizo kwa lengo la kuwafundisha wakulima, pia TARI walianzisha utaratibu wa kuanza maonyesho ya kilimo biashara ambayo huonyeshwa kwa kipindi chote cha mwaka.

Dk. Bucheyeki aliwahimiza wakulima kujifunza na kuzitumia teknolojia hizo ambazo walizibuni kwa lengo la kuwasaidia ili kuongeza uzalishaji wa mazao yao.





# Sababu kuchelewa kufungua madrasa zawekwa bayana

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISI ya Mufti Zanzibar imesema kuwa kuchelewa kufunguliwa kwa madrasa za Kurani haikuwa na nia ya kuuhujumu uislamu bali ni kuweka mazingira mazuri kwa walimu na wanafunzi.

Hayo yalielezwa jana na Katibu wa Mufti, Sheikh Khalid Ali Mfaume, alipokuwa akizungumza katika mkutano uliowakutanisha walimu wakuu wa madrasa ofisini kwake, Mjini Zanzibar.

Alisema baadhi ya watu wameitupia lawama taasisi hiyo yenye mamlaka ya kushughulikia masuala ya dini kwa kuchelewa kuzifungua madrasa ambazo zilifungwa tangu Machi, mwaka huu, kutokana na ugonjwa wa corona.

Sheikh Mfaume alisema watendaji wa ofisi hiyo walichelewa kuzifungua madrasa ili wapate nafasi ya kuweka mazingira mazuri kwenye madrasa hizo.

Aidha, alisema hatua ya serikali kutoa tamko la kufunguliwa kwa madrasa mwishoni mwa wiki, imetokana na kupungua kwa kiasi kikubwa cha maambukizi ya wagonjwa hao.

Madrasa nyingi za Zanzibar, alisema zimekuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi jambo ambalo ndilo lililosababisha kuchelewa kufunguliwa na tishio la kutokea kwa mlipuko wa corona.

Naye Mkurugenzi wa Utawala, Mipango na Rasilimali Watu wa Ofisi ya Mufti, Nouman Jongo, alisema ofisi imesikitishwa na vitendo vinavyofanywa na baadhi ya walimu wa madrasa kwa kuwadhalilisha watoto.

Alisema kumekuwa na tabia mbaya kwa baadhi ya watoto kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja jambo ambalo limesababisha kuporomoka kwa maadili.

**Kumekuwa na tabia mbaya kwa baadhi ya watoto kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja jambo ambalo limesababisha kuporomoka kwa maadili.**

# Mgombea urais ataka kampeni za kistaarabu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA wa urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ADA-TADEA, Juma Ali Khatib, ameahidi kufanya kampeni za kistaarabu zenye lengo la kuwaunganisha wananchi wa Zanzibar na kuwaletea maendeleo.

Khatib alisema hayo jana huko Bopwe, Wete kisiwani Pemba wakati akishiriki katika uzinduzi wa tawi la chama hicho ikiwa ni mikakati ya kuimarisha chama.

Aliwataka wananchi wa Pemba kuwakataa wanasiasa wenye uchu wa madaraka wakiwa na nia ya kupandikiza siasa za chuki ambazo hazina nafasi tena.

“Tunaingia katika ulingo wa harakati za kampeni hivi karibuni, lakini wito wangu kwa viongozi tufanye kampeni za kistaarabu zitakazowaunganisha wananchi na si kuwagawa kwani watu wetu wanataka maendeleo,” alisema.

**Nimejiunga na ADA-TADEA kwa matarajio yangu makubwa viongozi wetu watafanya siasa za kistaarabu zitakazowaunganisha wananchi wa Unguja na Pemba.**

Alisema kwa muda mrefu wananchi wa Pemba wameachwa nyuma kimaendeleo kwa sababu ya kuchagua viongozi wa vyama vya siasa ambao hawana nia njema ya kuwatumikia wananchi.

“Kwa bahati mbaya wananchi wa kisiwa cha Pemba kwa miaka mingi katika kipindi cha uchaguzi mkuu huchagua viongozi ambao hawana nia na maslahi ya kuwatumikia wananchi wa Unguja na Pemba,” alisema.

Katika upandishaji wa bendera katika tawi la Bopwe, wanachama 330 walijiunga na chama hicho baada ya kukihama Chama cha CUF na kile cha ADC.

Seif Shaaban Seif, mmoja wa mwanachama aliyejiunga na chama hicho kutoka CUF, alisema matarajio yake makubwa ni kuona uchaguzi mkuu wa Oktoba unafanyika katika mazingira ya amani huku viongozi wakiachana na jazba na chuki zinazoweza kuwagawa wananchi.

“Nimejiunga na ADA-TADEA kwa matarajio yangu makubwa viongozi wetu watafanya siasa za kistaarabu zitakazowaunganisha wananchi wa Unguja na Pemba,” alisema.

Katika ziara hiyo, Khatib akishiriki katika kazi ya wanachama kuchukua fomu kuomba nafasi za ubunge, uwakilishi na udiwani.



Mgombea wa nafasi ya urais wa Zanzibar kwa tiketi ya ADA-TADEA, Juma Ali Khatib, akipandisha bendera kuashiria uzinduzi wa tawi la chama hicho, huko Bopwe Wete Pemba jana, ikiwa ni hatua za kuimarisha chama kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, ambapo mgombea huyo alizindua zoezi la uchukuaji wa fomu za uwakilishi na ubunge. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waahidi ushindi wa kishindo CCM

**Na Rahma Suleiman,** PEMBA

WABUNGE watatu Kisiwani Pemba waliokihama Chama cha CUF na kujiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM), wamesema wamejitoa muhanga kuchukua uamuzi huo na watahakikisha wanakiletea ushindi chama hicho cha CCM kisiwani Pemba.

Wabunge hao waliomaliza muda wao, Mohamed Juma Ngwali (Wawi), Juma Hamad (Ole) na Kaizer Yussuf Makame (Chakechake), waliyasema hayo juzi katika mapokezi ya mgombea urais wa Zanzibar kupitia CCM, Dk. Hussein Mwinyi, Kisiwani Pemba.

Walisema Pemba imecheleweshwa kupata maendeleo kwa sababu wananchi wa kisiwa hicho walilishwa siasa za chuki na uhasama.

Makame alisema kwa sasa hakuna haja ya kuendeleza siasa hizo bali kuungana kuhakikisha Dk. Mwinyi anapata ushindi.

“Pemba ya leo si ile ya jana ambayo ilijaa siasa za chuki na uhasama. Hivi sasa ni Pemba ya kijani,” alisema.

Aidha, aliwataka wananchi wa kisiwa cha Pemba kubadilika na kuacha kuwachagua wapinzani ambao hawana walalowafanyia wananchi katika suala zima la maendeleo.

Kwa muda mrefu, alisema wapinzani wanachaguliwa katika uchaguzi mkuu, lakini wanaposhika nafasi zao hakuna anayekwenda katika jimbo lake kwa ajili ya kusimamia maendeleo.

Hamad ambaye aliwahi kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii katika serikali ya awamu ya pili ya Tanzania chini ya Rais (mstaafu) Ali Hassan Mwinyi, alisema huu ni mwaka wa wananchi wa Pemba kufanya uamuzi sahihi wa kuichagua CCM kushika hatamu ya kuongoza dola kwa kushika majimbo yote ya Pemba.

Alisema wananchi wa majimbo ya Pemba wamekosa maendeleo kwa sababu miaka yote wawakilishi hadi wabunge wanachagua kutoka upinzani ambao katika kipindi cha miaka mitano huwakimbia wapigakura.

Hamad alisema anamfahamu mgombea urais wa CCM Zanzibar na kwamba ana uwezo wa kutosha wa kuongoza Zanzibar na kuleta mabadiliko makubwa ya uongozi kwa kuwaunganisha wananchi wa Unguja na Pemba.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Abdalla Juma Sadalla, alisema wabunge wastaafu waliojiunga na CCM kutoka CUF watatumika kikamilifu kuhamasisha wananchi kukiunga mkono chama hicho na kupata ushindi wa kishindo.

Alisema kutokana na mapokezi makubwa ya wananchi wa kisiwa hicho kwa Dk. Mwinyi, aliwaahidi kuwa CCM itawalipa maendeleo wananchi wa kisiwa hicho.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**KULWA MASHIKU** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne chenye **index namba S.1841-0038** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KANDAWE SEKONDARI mwaka 2008. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Control No: **9910812949408.**

115818102

## KUPOTEA KWA KADI

**TATA AFRICA HOLDING TANZANIA LTD** inatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T668DHG** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato ya Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/CEN/RB/536118/2020**

115818502

## KUPOTEA KWA KADI

**TATA AFRICA HOLDING TANZANIA LTD** inatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T576DEM** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato ya Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/CEN/RB/536114/2020**

115818502

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**HAMIS RAJABU MKOGA** amepotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **HAOJUE** yenye namba za usajili **MC 360 CLU.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MOR/KIL/RB/534721/2020.**

115818402

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0782253676*

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Milioni 25 waambukizwa corona Iran

**TEHRAN,** Iran

RAIS wa Iran, Hassan Rouhani, amesema watu milioni 25 nchini humo tayari wamepata maambukizi ya virusi vya corona na wengine milioni 35 wako katika hatari ya kuambukizwa.

Kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Afya nchini humo, imetahadharisha kuwa nchi hiyo itahitaji idadi mara mbili zaidi ya vitanda. Mpaka sasa, idadi ya watu waliothibitishwa kuambukizwa ni 269,440.

**Maofisa wa afya walionya kulegeza masharti kunaweza kusababisha wimbi lingine la maambukizi ya corona.**

Rouhani alisema: "Ikiwa tutaitegemea ripoti hii, ambayo inasema watu milioni 25 nchini mwetu wameathirika na pengine idadi yote iliyobaki, karibu milioni 35 zaidi watapata maambukizi miezi ijayo, ripoti hiyo hiyo inakisia kuwa idadi ya watokaolazwa miezi ijayo inatarajiwa kuwa mara mbili zaidi ya ile tuliyoishuhudia siku 150 zilizopita."

Rouhani alisema watu 14,000 wamepoteza maisha kutokana na janga la virusi vya corona na 200,000 walilazwa hospitalini katika kipindi cha siku 150 zilizopita, kwa mujibu wa ripoti hiyo.

Misikiti kote nchini Iran ilifunguliwa miezi miwili iliyopita licha ya kwamba baadhi ya maeneo bado yalikuwa yameathirika vibaya na janga la virusi vya corona. Mikusanyiko ilikuwa imerejea katika miji 180 yenye kuonekana kuwa na kiwango cha chini cha hatari ya kupata maambukizi baada ya kukatizwa kwa miezi miwili kulingana na kituo cha habari cha taifa hilo.

Iran pia iliondoa marufuku ya kusafiri baina ya miji na majengo ya kibiashara huku shughuli za kibiashara zikiwa zimerejelewa.

Iran, moja ya maeneo ya Mashariki ya Kati yaliyoathirika vibaya na virusi vya corona, ilianza kulegeza masharti na kurejelea maisha ya kawaida ili kufufua uchumi ambao tayari unakumbana na vikwazo vya Marekani.

Hata hivyo, maofisa wa afya walionya kwamba kulegeza masharti kunaweza kusababisha wimbi lingine la maambukizi ya virusi vya corona. **BBC**



Wanachama wa chama cha upinzani nchini Mali, wakiwa katika maandamano wakishinikiza kujiuzulu kwa Rais wa nchi hiyo, Ibrahim Boubakar Keita. **PICHA: REUTERS**

## Upinzani waitisha maandamano kumpinga rais

**BAMAKO,** Mali

IDADI kubwa ya wananchi nchini Mali hususani kutoka chama cha upinzani wamefanya maandamano ya kumkataa Rais wa nchi hiyo, Ibarahim Boubakar Keita.

Rais Keita ambaye amesalia na miaka mitatu tu katika muhula wake wa mwisho, anakabiliwa na shinikizo za kutaka ajiuzulu tangu mwanzoni mwa mwezi Juni. Umaarufu wake umeshuka kutokana na madai ya ufisadi yanayoizonga serikali yake, huku mzozo wa wapiganaji wa Kiislamu wenye itikadi kali ukiendelea kuitia doa serikali yake.

Wito wa kumtaka Rais Keita kujiuzulu umeongezeka baada ya maandamano ya hivi karibuni kujibiwa vikali na vikosi vya usalama na kusababisha kifo cha kiasi ya watu 12.

Maandamano hayo yalisitishwa kwa muda wakati wa mazungumzo na wapatanishi 15 kutoka Jumuiya ya Kiuchumi ya Mataifa ya Afrika Magharibi (ECOWAS), lakini muungano wa upinzani unaofahamika kama Juni 5 umeitisha tena maandamano baada ya kuukataa mpango wa ECOWAS. **DW**

## Trump, seneti kujadili mapambano corona

**WASHINGTON,** Marekani

VIONGOZI wakuu wa Chama cha Republican katika Bunge la Marekani, wanatarajiwa kukutana na Rais Donald Trump, kujadili mpango mwingine wa msaada wa kifedha unaonuwia kupunguza mtikisiko uliosababishwa na ugonjwa wa virusi vya corona.

Mkutano huo unatarajia kufanyika katika Ikulu mjini Washington umeitishwa wakati matumaini ya Wamarekani kuwa janga la virusi vya corona linaelekea ukingoni.

Migawanyiko baina ya viongozi wakuu wa Chama cha Republican katika Baraza la Seneti na Ikulu ya Marekani inatishia kuleta changamoto mpya katika kushughulikia kadhia ya corona.

Kiongozi wa Republican katika Baraza la Seneti, Mitch McConnell, alitaka kuwako mpango mwingine wa uokozi wa dola trilioni moja katika siku chache zinazokuja, lakini utawala wa Rais Trump unatoa kipaumbele katika kuongeza fedha za kuimarisha upimaji wa virusi vya corona.

Jana, Rais Trump alilisitiza kuwa virusi vya corona vitatokomezwa hivi karibuni lakini maoni yake yanatofautiana na makadirio ya wataalamu wa afya wanaotiwa wasiwasi na ongezeko la visa vipya na vifo nchini humo.

Wakati matukio ya maambukizi ya virusi vya corona ikifikia milioni 14 kote duniani, Marekani tayari imerekodi visa 3,762,081 nchini nzima.

Nchini India moja ya Taifa lililoathiriwa na ugonjwa wa corona, serikali imetangaza maambukizi mapya 40,000 ya virusi vya corona vilivyorekodiwa katika muda wa saa 24 zilizopita.

Idadi hiyo ambayo ni kubwa zaidi kuwahi kuripotiwa inafanya India kufikia maambukizi 1,118,043 na vifo 27,497 vya corona.

Wakati hayo yanajiri barani Asia, nchini Brazil, Taifa la Amerika ya Kusini idadi ya vifo vya corona inaelekea kufikia 80,000 baada ya watu 716 kupoteza maisha Jumamosi pekee. **DW**

## Majambazi yaua wanajeshi 23

**LAGOS,** Nigeria

GENGE la majambazi kutoka kijiji cha Kaskazini Magharibi mwa Nigeria limewaua wanajeshi 23 nchini Nigeria.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa majambazi hao waliwafyatulia risasi wanajeshi waliokuwa wakitembea kwa miguu karibu na eneo lenye misitu katika Wilaya ya Jibia, Jimbo la Katsina.

Kwa mujibu wa chanzo cha jeshi, miili ya wanajeshi 23 imepatikana japo kuna wengine ambao hawajulikani walipo.

Idadi ya wanajeshi waliouawa huenda ikaongezeka kwa sababu zoezi la kutafuta wanajeshi wengine linaendelea.

Magenge ya watu wenye silaha yamekuwa yakihusika na wizi wa mifugo na utekaji nyara, lakini wataalamu kadhaa wanaonya kuwa huenda wanashirikiana na makundi ya Jihadi katika eneo hilo.

Vile vile, Jumamosi watoto watano waliuawa na wengine sita walijeruhiwa katika eneo hilo baada ya bomu kulipuka kimakosa, alisema msemaji wa Jeshi la Polisi katika Jimbo hilo la Katsina. **DW**

# MOURINHO: KANE HAWEZI KUWA SPESHO NJE YA SPURS




**LONDON,** England

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho amedai Harry Kane "hatakuwa mtu muhimu akicheza katika timu nyingine" huku kukiwa na uvumi juu ya majaliwa yake ya baadaye hapo Spurs.

Kane alifunga mabao mawili mfululizo wakati Tottenham ikiikuba na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Leicester City na kufufua matumaini ya kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Baada ya kufunga katikati ya wiki kwenye ushindi wa 3-1 dhidi ya Newcastle United, Kane tena alifunga mara mbili kabla ya kipindi cha pili dhidi ya Leicester jijini London baada ya James Justin kujifunga dakika ya sita ya mchezo huo.

Kane awali alikataa kuondoa uwezekano wa kuondoka Tottenham, lakini kocha huyo wa Spurs, Mourinho amemuonya nyota huyo wa England anaweza asipate nafasi sawa kama ilivyo sasa akienda sehemu nyingine.

"Nafikiri kila mmoja anafikiria kwamba yeye ni mchezaji anayevutia na Tottenham wana bahati kubwa kuwa naye kwa sababu yeye ni mchezaji, mtu na kijana wa Tottenham," alisema Mourinho akiwaambiwa waandishi wa habari.

"Yote hayo yanamfanya yeye kuwa mchezaji wa aina yake kwa upande wetu, pengine hali haitakuwa hivyo kama akicheza kwa timu nyingine.

"Ni mtu spesho kwetu, kwa hakika kabisa ni spesho kwa Tottenham.

"Bila shaka tunataka yeye awe na furaha ili aweze kuwa na furaha unatakiwa ushindi, kufunga mabao na nina furaha baada ya kutoka kwenye majeraha yaliyomuweka nje. Matumaini yangu ataanza vizuri zaidi msimu ujao akiwa bora kabisa."

Kane amefunga mabao 17 kwenye Ligi Kuu msimu huu, akipitwa sita kwenye mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu na nyota wa Leicester, Jamie Vardy, huku ukiwa umebakiwa mchezo mmoja ligi kumalizika."



# Arsenal itavutia wapya - Arteta

**LONDON,** England

MIKEL Arteta bado anaamini Arsenal ina nafasi ya kuvutia usajili wa wachezaji wapya, kwa sababu klabu hiyo "inaweza kupigania" taji.

'Washikabunduki' hao walikabiliwa na wakati mgumu msimu huu wa 2019-20, ikiwamo kubadili kocha baada ya kuondoka kwa Unai Emery, Novemba, lakini imeonyesha kuimarika katika siku za hivi karibuni chini ya Arteta.

Baada ya ushindi dhidi ya mabingwa wa Ligi Kuu ya England, Liverpool katikati ya wiki, Arsenal ilirekodi ushindi wa 2-0 dhidi ya Manchester City kwenye nusu fainali ya Kombe la FA, ikiwa na uwezekano wa kubeba taji na pia kufuzu kucheza Ligi ya Europa msimu ujao.

Matokeo hayo mawili yameifanya timu hiyo kuonyesha kuwa na kiwango cha kuvutia chini ya kocha huyo raia wa Hispania, ambaye anahisi klabu inaweza kumvutia mchezaji yeyote yule.

"Nilisema hapo kabla kwamba sifikirii kuleta wachezaji wengi ambao tutalazimika kuwashawishi," alisema Arteta akiviambia vyombo vya habari.

"Hii ni klabu yenye nafasi kubwa ya kuwavutia wachezaji na si lazima hadi uwashawishi.

"Hisia nilizonazo wakati nazungumza naona kuna wachezaji wengi wanaweza kuja hapa, kwa sababu ya historia ya klabu, namna tunavyofanya mambo mengi, thamani yetu, mashabiki na mashabiki tulioano.

"Vitu vyote hivi vinavutia kwa uhakika kabisa."

# Messi aweka rekodi ufungaji bora LaLiga

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi ameweka historia ya kutwaa kwa mara ya saba 'Pichichi' kwenye Ligi Kuu ya Hispania, baada ya kumaliza msimu wa 2019-20 akiwa mfungaji bora kwenye LaLiga.

Nyota huyo wa Argentina aliifikia rekodi ya gwiji wa Athletic Bilbao, Telmo Zarra ya kuitwaa tuzo hiyo mara sita msimu uliopita, lakini kwa sasa yupo katika dunia ya peke yake.

Mabao yake mawili kwenye ushindi wa 5-0 dhidi ya Deportivo Alaves yalimfanya kufikisha mabao 25 katika mechi 33 za Ligi Kuu msimu huu, kwenye mechi hiyo iliyokuwa ya mwisho LaLiga.

Hata hivyo, mabao hayo hayakutosha kuiwezesha Barca kutwaa taji la tatu mfululizo la Ligi Kuu, huku Real Madrid wakiubeba ubingwa huo.

Mshambuliaji wa Madrid, Karim Benzema amepitwa mabao manne baada ya kufikisha 21, huku nyota wa Villarreal, Gerard Moreno ambaye amefikisha mabao 18, akimpita mawili mchezaji mwenzake na Messi pale Barca, Luis Suarez.



# Hazard: Msimu huu umekuwa mbaya kwangu

**MADRID,** Hispania

EDEN Hazard amekubali kwamba mwaka wake wa kwanza pale Real Madrid umekuwa mbaya zaidi katika maisha yake ya soka.

Nyota huyo wa zamani wa Chelsea aliwagharimu Madrid ada ya awali ya euro milioni 100 Julai mwaka jana, lakini amekabiliwa na majeraha ya mara kwa mara kwa kipindi kirefu cha msimu huu wa 2019-20.

Maumivu ya nyama za paja yalimfanya achelewe kuanza kuwachezea Los Blancos hao, huku maumivu ya kifundo cha mguu yakachangia kumfanya aanze katika mechi 21 tu kwenye mashindano yote msimu huu.

Madrid wameshinda taji la Supercopa de Espana na LaLiga mwaka 2019-20 na bado ipo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, ingawa kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya 16 walifungwa na Manchester City 2-1.

"Nilikuwa na majeraha ya muda mrefu, lakini natumaini mwakani nitakuwa bora zaidi," alisema Hazard, ambaye aliachwa kwenye kikosi kilichoivaa Leganes Jumapili, akiiambia franceinfo.

"Hata kama msimu huu ulikuwa mbaya kwa upande wangu, nisingeweza kufanya lolote, lakini naamini mwakani nitakuwa kwenye wakati mzuri zaidi.

"Mwaka huu ni mzuri kwa sababu tumeshinda taji la ligi, kila mmoja ametoa mchango mkubwa kwa timu na kwa uhakika kabisa nilikuwa na msimu mbaya zaidi katika maisha yangu ya soka."

Kama Madrid wataweza kupindua matokeo dhidi ya City, watakutana na Juventus au Lyon kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mjini Lisbon.






# LAMPARD ASIFU KIWANGO CHELSEA

**LONDON,** England

FRANK Lampard amesifia ubora na kiwango cha kikosi chake cha Chelsea baada ya kuifumua Manchester United mabao 3-1 na kutinga fainali ya Kombe la FA.

Olivier Giroud na Mason Mount kila mmoja alifunga bao kipindi cha kwanza katika mchezo huo uliopigwa kwenye dimba la Wembley - wakitumia makosa ya golikipa David de Gea na Harry Maguire akajifunga na kuwapa bao la tatu Chelsea.

Ushindi huo umekuja si zaidi ya wiki baada ya Lampard kukishutumu kikosi chake kwa kuonyesha kiwango kibovu wakati wakichezea kichapo cha mabao 3-0 kwenye Ligi Kuu kutoka kwa Sheffield United.

Lakini kocha huyo wa Chelsea anaona wachezaji wake walionyesha kiwango cha kuvutia zaidi dhidi ya Man United wakati walipoutawala mchezo huo na sasa wanawavaa wapinzani wao wa jiji moja Arsenal, Agosti Mosi mwaka huu.

"Siwezi kuomba zaidi kutoka kwa wachezaji wangu zaidi ya pale kiwango walichoonyesha na namna walivyokuwa na ari kubwa," alisema akiiambia BBC Sport.

"Tulikuwa juu na wakati walipobadili staili yao ya uchezaji tulikuwa bora zaidi. Najisikia fahari kubwa kwa kiwango walichokionyesha.

# Emery kuwa kocha mkuu Villarreal

**VALENCIA,** Hispania

UNAI Emery yupo kwenye mazungumzo ili kuwa kocha mkuu mpya wa klabu ya Villarreal, vyombo vya habari vya Hispania vimeripoti.

Emery anatarajia kurudi tena kwenye kazi ya ukocha na nafasi hiyo inaonekana kuelekea kule Villarreal. Raia huyo wa Hispania amekuwa hana kazi tangu alipofukuzwa na Arsenal Novemba mwaka jana.

Kocha wa sasa wa klabu hiyo, Javier Calleja anaondoka pale Villarreal akiacha ikiwa nafasi ya tano kwenye msimamo wa La Liga, na alipoulizwa kuhusu majaliwa yake wiki hii alisema: "Sijui kuhusu majaliwa yangu ya baadaye.

"Nini kitakachotokea kitaamuliwa na klabu. Nina mahusiano mazuri na klabu, na nina furaha kupata nafasi ya kufikiriwa na Villarreal.

"Nitaendelea kufanya kazi kwa bidii kwa Villarreal, na kuwaacha wengine wafanye maamuzi."

Emery alichukua nafasi ya Arsene Wenger kama kocha wa Arsenal, Mei mwaka 2018 na aliiongoza klabu hiyo kwenye fainali ya Ligi ya Europa na kumaliza nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu.

Alifukuzwa Novemba mwaka 2019 na nafasi yake ilichukuliwa na Freddie Ljungberg kwa muda kabla ya kuteuliwa kwa Mikel Arteta.

Emery aliwahi kuwanoa wapinzani wakubwa wa Villarreal, Valencia msimu wa 2008-2012.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER: NILIIPANGIA CHELSEA KIKOSI DHAIFU

●●● Tulichagua timu ambayo ingetuwezesha kushinda, lakini haikufanya kazi...

**LONDON,** England

OLE Gunnar Solskjaer amekubali uchaguzi wa timu yake dhidi ya Chelsea "haukufanya kazi" wakati alipowapumzisha nyota wake muhimu kwenye kipigo cha nusu fainali ya Kombe la FA.

**David de Gea alifanya makosa mara mbili wakati Chelsea walipomaliza umwamba wa Manchester United wa kutopoteza mechi kwa muda mrefu, na kukubali kichapo cha mabao 3-1 pale kwenye dimba la Wembley na kufuzu fainali ya FA ambayo watakutana na Arsenal.**

United ambao walikuwa wamecheza mechi 19 bila kupoteza kwenye mashindano yote walianza bila Paul Pogba, Anthony Martial na Mason Greenwood wakati Solskjaer alipofanya mabadiliko manne kutoka kikosi kilichoshinda dhidi ya Crystal Palace.

Alilazimika kufanya mabadiliko kabla ya Chelsea kupata bao la kuongoza wakati Eric Bailly alipotolewa nje kwa kuumia kichwa.

Bosi huyo wa United alikubali kwamba jicho moja lilikuwa linautazama mchezo unaofuata wa Ligi Kuu dhidi ya West Ham utakaopigwa kesho Jumatano wakati akichaguo kikosi chake cha kwanza.

Alisema: "Tulichagua timu ambayo ingetuwezesha kuwa na nafasi bora kuendelea kwenye mchezo wa Jumatano. Lakini haikufanya kazi. Tukalazimika kubadilisha mambo kipindi cha pili wakati Eric alipotolewa nje. Nilichagua timu ambayo ingeweza kupenya kwenye nusu fanali."

De Gea anaendelea kuwa kwenye presha kubwa kuhusu nafasi yake hapo United baada ya kufanya makosa kadhaa yanayoigharimu timu, na alifanya makosa mawili yaliyosababisha Olivier Giroud kufunga bao na Mason Mount.

"Kila mmoja anatakiwa kuwa kwenye kiwango chake na kila mmoja ana nafasi ya kushutumiwa," alisema Solskjaer. "David alijua kwamba angeweza kuokoa bao la pili, lakini hilo limeshatokea. Ni ngumu kwa golikipa kufidia makosa yake. Ni rahisi zaidi kwa mchezaji mwingine ndani ya dimba. Alionyesha katika sehemu nyingine ya mchezo kwamba, alifanya vizuri kwa kuokoa hatari kadhaa, lakini David anajua kwamba angeweza kuokoa nyingine.

"Kwa sasa akili tunaielekeza katika mchezo wa Jumatano usiku dhidi ya West Ham kwenye Ligi Kuu ya England."

## ZISIKUPITE

### SANCHO ANUKIA UNITED

WINGA wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20, sasa anaweza kuanza uhamisho wake wa kwenda Manchester United akiweka wazi kuwa anataka kuondoka katika klabu hiyo ya Ujerumani. ***(Mirror)***

### JUVE KUMTOA COSTA

JUVENTUS inakaribisha ofa kutoka Manchester City na Paris St-Germain kwa ajili ya mshambuliaji Mbrazil Douglas Costa mwenye umri wa miaka 29, na wanataka nafasi yake irithiwe na straika wa Wolves na Mexico, Raul Jimenez mwenye miaka 29. ***(Tuttosport)***

### CEBALLOS ANOGEWA ARSENAL

KIUNGO wa Arsenal, Dani Ceballos mwenye umri wa miaka 23, yupo tayari kumuomba Rais wa Real Madrid, Florentino Perez kuongeza muda wa kucheza kwa mkopo pale Arsenal kwa msimu mwingine. ***(El Confidencial)***

### MARCELO, LEEDS KUTETA

KLABU ya Leeds itafanya mazungumza ya mkataba na kocha wa Argentina, Marcelo Bielsa wiki hii. ***(Star)***

### KLUIVERT AWINDA BARCA

STRAIKA wa zamani wa Barcelona na Uholanzi, Patrick Kluivert na mshindi wa Kombe la Dunia na Ufaransa mwaka 1998, Laurent Blanc, ambaye aliinoa Bordeaux, Ufaransa na PSG, wanaongoza mbio za kuchukua mikoba ya ukocha pale Nou Camp kama Quique Setien akifukuzwa. ***(AS)***

### LUIZ KUMBADILI ARTETA

KUIMARIKA kwa kiwango cha mlinzi wa Arsenal na Brazil, David Luiz mwenye umri wa miaka 33, kunaweza kubadili mtazamo wa Mikel Arteta wakati wa usajili wa dirisha la majira ya joto. ***(Star)***

### BAYERN YATUA WEST HAM

KIUNGO wa West Ham, Benicio Baker-Boaitey mwenye umri wa miaka 16, anajiandaa kujiunga na Bayern Munich na atasafiri kwenda Ujerumani kwa mazungumzo, akiwa amekataa nafasi ya kusaini mkataba mpya na wagonga nyundo hao wa London. Januari atatimiza umri wa miaka 17. ***(Sun)***

### WILLIAN AISUBIRIA CHELSEA

KIUNGO wa Chelsea, Willian mwenye umri wa miaka 31, raia wa Brazil, amekuwa akihusishwa na Tottenham, Arsenal na Manchester United, amebainisha kwamba anasubiria kusaini mkataba mpya pale Stamford Bridge, akiwa anataka miaka mitatu na klabu imempa ofa ya miaka miwili. ***(De Sola, via Mirror)***

### KOCHA NEWCASTLE AHOFU

KOCHA Mkuu wa Newcastle United, Steve Bruce anahofia bajeti ya usajili ya klabu itakatwa kwa sababu mapato ya pauni milioni 170 ya mwaka jana yatashuka. ***(Mirror)***

### MCGINN KUTUA ASTON VILLA

NEWCASTLE inapanga kuingia kwenye usajili kwa kumsajili kiungo wa Aston Villa, John McGinn mwenye umri wa miaka 25, raia wa Scotland. ***(Birmingham Mail)***

HABARI MICHEZO

## Alliance hasira kwa Ndanda, Namungo

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Alliance FC, Kessy Mziray amesema wamekikubali kichapo kutoka kwa Simba na sasa wanapambana kuhakikisha wanatumia vema uwanja wa nyumbani katika mechi mbili zilizobaki ili wainusuru timu yao na kuiwezesha kuwamo Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Juzi ikiwa katika Uwanja wa Taifa, Alliance ilikubali kipigo cha mabao 5-1 kutoka kwa Simba, matokeo ambayo yanaifanya kushika nafasi ya nne kutoka mkiani ikiwa na alama 41.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mziray alisema Simba wametumia makosa waliyoyafanya kuwaadhibu na kupata ushindi huo mkubwa.

Alisema Simba walitumia nafasi zao vizuri na kupata ushindi huo na kwamba licha ya wao kupata nafasi, lakini hawakuweza kuzitumia kwa mafanikio.

"Tumemaliza mechi na Simba, sasa nguvu na akili zetu ni kupambania timu kufanya vizuri katika mechi zetu mbili kupata matokeo mazuri ili kuinusuru timu na kuweza kubaki Ligi Kuu," alisema Mziray.

Alisema wapo katika hali mbaya ya wasipokuwa makini kutafuta alama muhimu katika mechi timu inaweza kushuka daraja.

"Tunaenda kufanyia kazi mapungufu yetu yasijirudie tena katika mechi hizo mbili kuhakikisha tunapata pointi muhimu zitakazotufanya kubaki Ligi kUU," alisema kocha huyo.

Alliance kwa sasa imebakiza mechi mbili dhidi ya Ndanda FC kesho kutwa katika Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza kabla Julai 26, mwaka huu kuhitimisha kwa kuikaribisha Namungo FC.

## Mgeveke: Msimu huu mgumu zaidi

**Na Shufaa Lyimo**

LICHA ya nahodha wa Klabu ya Mwadui FC, Joram Mgeveke kueleza siri ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Yanga katika mchezo wa Ligi Kuu uliopita kuwa ni umakini walionao wachezaji pamoja na kufuata maelekezo ya kocha wao, Khaled Adam, amekiri kuwa huu ndio msimu mgumu zaidi kwake kuwahi kuushuhudia kwenye ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mgeveke alisema walipanga kuondoka na pointi zote tatu katika mchezo huo na kama ikishindikana wapate pointi moja jambo ambalo lilifanikiwa.

"Sisi wachezaji tulipanga tupambane tupate pointi tatu tukiwa ugenini kama ikishindikana turudi nyumbani na pointi moja jambo ambalo limewezekana, sasa hivi tunajipanga kukutana na Biashara United kesho," alisema Joram.

Nahodha huyo alisema kwa upande wake msimu huu umekuwa mgumu tofauti na msimu uliopita, kwa madai kuwa kila timu imejipanga kufanya vizuri na kwamba tangu aanze kucheza soka huu ndio msimu mgumu zaidi kuwahi kuushuhudia Ligi Kuu.

# JKU HAKUNA KULALA HADI KIELEWEKE UBINGWA Z'BAR

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa JKU, Omar Khamis "Matu" amesema hawatabweteka kwa ushindi walioupata wa mabao 4-0 dhidi ya Chipukizi katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar juzi na badala yake wataendelea kucheza kwa tahadhari kubwa watakapoivaa Machomane leo na timu zingine zilizopo katika ukanda wa kushuka daraja.

**Kwa ushindi huo wa juzi, JKU imeendelea kupaa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama 61.**

Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi hiyo iliyopigwa katika Uwanja wa Mau A kisiwani hapa, Matu alisema lengo lao ni kuhakikisha michezo yote iliyobaki inapata ushindi ili kuendelea kujiweka katika mazingira mazuri ya kutwaa ubingwa wa Zanzibar ambao hadi sasa hakuna timu inayoweza kujihakikishia kuutwaa.

Kocha huyo alisema kwa sasa wanacheza kwa tahadhari kubwa na kwa umakini ikiwamo dhidi ya timu ambazo zipo ukanda wa kushuka daraja kwani michezo yao ndiyo inayokuwa migumu zaidi.

"Ligi ni ngumu sana, lakini wachezaji wa timu zote wanapambana ili kuhakikisha wanapata matokeo mazuri na hata wachezaji wengine kupambana kwao ni kukwepa lawama za uwanjani kama walifanya vibaya na kuzisababishia timu kukosa alama tatu hususan katika kipindi hiki cha kuelekea ukingoni mwa ligi," alisema.

Aidha, alisema kuwa mchezo wao wa leo dhidi ya Machomane amejiandaa kupata alama tatu ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kuutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu.

Katika mechi hiyo ya juzi, mabao ya JKU yalifungwa na Mnageria Shehu Magaji Bulama dakika ya 19, Ahmed Ali Omar (dk 44), Mustafa Hamad Simai dakika ya 80 na 87.

Ligi hiyo inatarajiwa kumalizika Julai 30, mwaka huu huku jumla ya timu sita zikishuka daraja.




Kiungo Luis Miquissone (kushoto) na mshambuliaji Meddie Kagere miongoni mwa mashujaa wa Simba walioipa ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya Alliance katika Uwanja wa Taifa juzi. Simba itashuka tena dimbani keshokutwa, Jumatano kuivaa Coastal Union katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga. **PICHA: SIMBA**

# *Daraja la Kwanza Unguja sasa Agosti*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LIGI Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja inatarajiwa kuendelea kutimua vumbi Agosti 6, mwaka huu baada ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuruhusu kuendelea kwa michezo mingine ikiwa ni pamoja na mashabiki kuruhusiwa kuingia uwanjani.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Mkurugenzi wa Mashindano wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF), Ali Mohammed Ameir, alisema ligi hiyo itaendelea kama ilivyokuwa hapo awali katika viwanja viwili vya Mau A pamoja na Mau B.

Alisema kwa upande wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja inamichezo michache ikilinganishwa na Kanda ya Pemba, hivyo Kamati ya Mashindano itaangalia namna ya kupanga ratiba ili imalize kwa wakati na kupata timu itakayopanda daraja kucheza Ligi Kuu msimu ujao.

"Serikali imetoa ruhusa ya kuendelea kwa ligi nyigine, hivyo Kamati ya Mashindano, tunaendelea na kupanga ratiba pamoja na kuzingatia mambo yote ambayo serikali imeyaelekeza katika kuendelea kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona," alisema.

Aidha, alisema ligi zote zinazosimamiwa na ZFF, mikoa pamoja na wilaya zinaendelea kulingana na ratiba zao ili kuzipata timu zitakazopanda madaraja katika msimu mpya wa ligi wa 2020/2021.

Hata hivyo alisema kwa upande wa Ligi Daraja la Kwanza, timu zitapewa wiki mbili za maandalizi kabla ya kurudi dimbani.

Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja inajumuisha timu 13 wakati kwa pande wa Kanda ya Pemba ikiwa na timu 18.

Michezo
Jumanne Julai 21, 2020
Nipashe



Solskjaer: Niliipangia Chelsea kikosi dhaifu UKURASA 22

FUNGA MSIMU...




Mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi (kulia) akimiliki mpira katika mechi ya funga msimu wa LaLiga dhidi ya Deportivo Alaves alipoifungia mabao mawili wakati wakishinda 5-0 kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Mendizorroza juzi usiku. Mabao mengine yalifungwa na Ansu Fati, Luis Suarez na Nelson Semedo. **PICHA: MTANDAO**

# SABA ZACHUNGULIA SHIMONI LIGI BARA

## ● ● ● Ndanda FC, Alliance FC, Mwadui, Lipuli FC, Mtibwa Sugar na Mbeya City sasa zinahitaji...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI zikiwa zimebaki raundi mbili tu Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2019/20 umalizike, jumla ya timu saba zipo kwenye hatari zaidi ya kushuka daraja kama zisipofanya vema kwenye mechi zilizobaki.

**Kulingana na msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, timu zinazochungulia 'kaburi' ambazo huenda msimu ujao zisiwapo ni Mbao FC, Ndanda FC, Alliance FC, Mwadui FC, Lipuli, Mtibwa Sugar na Mbeya City.**

Timu hizi zisipochanga karata zao vizuri basi tatu kati ya hizi zitaungana na Singida United kucheza Ligi Daraja la Kwanza msimu ujao, lakini mbili zitakwenda kucheza mechi za mchujo na kama zikifungwa basi ndiyo zitakuwa zimeshuka moja moja na kama zikishinda, basi zitarejea Ligi Kuu msimu ujao.

Baada ya mechi za mwishoni mwa wiki, ikishuhudia Simba ikiwa ndiyo timu pekee iliyoshinda mechi yake nyumbani kwa kuitwanga Alliance FC mabao 5-1, mechi tisa zilizobaki zote hakuna timu yoyote iliyoshinda nyumbani.

Ukiacha Singida ambayo tayari imeshashuka daraja, timu iliyo juu yake ni Mbao FC ambayo sare ya bao 1-1 dhidi ya JKT Tanzania bado imeifanya kubaki kwenye nafasi yake hiyo hiyo ya kudumu ya 19, licha ya kushinda mechi tano mfululizo na sare moja, sasa ikifikisha pointi 39.

Timu nyingine iliyo kwenye hatari ya kushuka au kucheza mechi za mchujo ni Ndanda FC ambayo ilichapwa nyumbani bao 1-0 dhidi ya Mbeya City, imebakiwa na pointi 40, ikiwa kwenye nafasi ya 18.

Baada ya kukandikwa mabao 5-1, Alliance inabakia na pointi 41, ikikamata nafasi ya 17 ambayo nayo si salama na inahitaji pointi zote sita ili ifikishe pointi 47, huku ikisubiri matokeo ya timu zingine.

Mwadui FC, licha ya kuikomalia Yanga na kwenda nayo sare ya bao 1-1, iko kwenye hali mbaya, nafasi yake ya ni ya 16, kwa pointi zake 41.

Lipuli nayo pia ina pointi 41, lakini inashika nafasi ya 15, nayo haipo kwenye nafasi nzuri, kinachotakiwa ni juhudi tu ya kushinda mechi zake mbili zilizobaki, halafu kuangalia matokeo ya wenzake pia.

Mtibwa Sugar ambayo wiki hii ilichapwa nyumbani bao 1-0 dhidi ya KMC, imebakiwa na pointi zake 41, ikishika nafasi ya 14 na kuwafanya wapinzani wao kujiweka salama kwenye eneo hatari.

Nafasi nyingine ya hatari ya kushuka daraja, au kwenda kucheza mechi za mchujo na timu zilizoshika nafasi za pili kwenye Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara, imeshikiliwa na Mbeya City, kwani licha ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Ndanda, lakini pointi zilizonazo 42, bado hazitoshi kuifanya ibaki Ligi Kuu kama haitoongeza pointi zingine sita kwenye mechi zilizobaki.

# Yanga hasira kwa Mtibwa

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI Yanga ikielekea mkoani Morogoro jana tayari kwa mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Mtibwa Sugar, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mbelgiji Luc Eymael amesema anachokitaka ni ushindi tu ili kujihakikishia kumaliza nafasi ya pili msimu huu.

Yanga inayoshika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na alama 68 mbili mbele ya Azam FC wanaowafukuzia kwa kasi, itahitaji ushindi ili kuzidi kujihakikishia kumaliza katika nafasi hiyo, lakini Mtibwa Sugar nayo itahitaji ushindi ili kujinusuru na janga la kushuka daraja.

Eymael akizungumza na Nipashe jana, baada ya mazoezi ya asubuhi kwenye Uwanja wa Chuo cha Sheria, Ubungo jijini Dar es Salaam, alisema wachezaji wake wako vizuri kuelekea katika mchezo huo, na anaamini wanaweza kupata ushindi huku akiwataka kuzidisha umakini uwanjani.

"Tumemaliza mazoezi salama wachezaji wangu wanaendelea vizuri, na kwa mujibu wa uongozi muda mfupi kuanzia sasa (jana saa nne) wachezaji watakwenda kambini kwa ajili ya kujiandaa na safari kuelekea Morogoro lengo ni kurudi na pointi tatu.



Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila (pichani), akizungumza na gazeti hili kwa simu kutoka mjini Morogoro, alisema mchezo huo unampasua kichwa kwa kuwa anaamini utakuwa na ushindani mkubwa huku wakihitaji kushinda kutokana na nafasi waliyopo kwa sasa.

Alisema msimu huu kwa upande wao umekuwa mgumu, kutokana na matokeo ambayo hayaridhishi kwenye michezo ambayo wamecheza.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >